# Nipashe

Alhamisi Juni 4, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580249

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Sababu Tanzania kusitisha shughuli mpakani Namanga

UKURASA 3


ama

AFYA NA MAZINGIRA

Corona 'kupumua' ina ujumbe gani kwa safari kuu ya afya?

Kwa nini mtu anatoa harufu kinywani, koo lahifadhi jiwe?

Bosi Mkuu TFS: Tumenufaika na misitu, vikwazo vyetu hivi...

Hatimaye, vita fistula imeanza kuwasha taa ushindi kimataifa

• Nchi imevuka mstari wa mafanikio

UKURASA 11

# Chadema yafungua milango urais Oktoba

**WATIA** nia kujitokeza hadi Juni 15, vyama vyaitwa kuunda ushirikiano... *Endelea ukurasa 2*



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dk. John Magufuli, akijadiliana jambo na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, baada ya kikao chao Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma jana. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Philip Mangula. **PICHA: IKULU**

## BAA LA CORONA



Kwa nchi ambazo tayari zimekumbwa na ugonjwa wa Covid-19, mambo muhimu ya kuzingatia kunapokuwa na mwingiliano wa watu kutoka nje ni kuwalinda washiriki wa nchi zingine wasipate maambukizo. WHO

* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## MAGUFULI, DK. SHEIN, BASHIRU, MANGULA WATETA

UKURASA 4

# Watatu walivyotiwa mbaroni mauaji ya dereva teksi Dar

UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store



**MICHEZO** SIMBA SC KUTANGAZIA UBINGWA NANGWANDA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA



Wakili wa Shirika la Civic and Legal Aid Organization (CILAO), Paul Kaunda (kulia), akizungumza na Wakili wa Serikali, baada ya kesi ya kikatiba aliyoifungua katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam ya kuomba tafsiri ya kisheria kufuatia kitendo cha Spika Job Ndugai, kumrejesha Bungeni, Mbunge Cecil Mwambe, kutupiliwa mbali na mahakama hiyo, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Chadema yafungua milango watia nia urais

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimefungua milango ya wagombea wa nafasi ya urais kutia nia kupitia chama hicho kuanzia leo hadi Juni 15, mwaka huu.

Pia, chama hicho kimefungua milango ya majadiliano ya ushirikiano kuelekea katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu, kwa vyama vingine vya siasa.

"Mlango ambao tumeufungua leo ni wa kuruhusu watia nia ya urais wa Tanzania kupitia tiketi ya Chadema. Na tunafungua pia mlango na vyama ambavyo vina dhamira ya dhati na kweli ya kushirikiana kuiondoa CCM madarakani ili viingie kwenye majadiliano na sisi ya ushirikiano huo," alisema Mnyika.

Akitoa maelekezo kwa watia nia wa nafasi ya urais kupitia chama hicho, Mnyika alisema katika hatua hiyo ni vyema watia nia hao wakazingatia Katiba, taratibu na miongozo ya chama hicho.

"Ni vyema watia nia wakarejea kwamba chama chetu kinaendeshwa kwa Katiba, kanuni, maadili, itifaki, taratibu. Chama kinao mwongozo wa kutangaza kusudio la kuwania nafasi za uongozi kwenye vyombo vya uwakilishi serikalini."

"Na katika mwongozo huu, pamoja na mambo mengine, umetaja utaratibu wa kusudio hilo la kutangaza nia ya kugombea ambao kipengele cha 1(g) cha mwongozo kinatamka kwamba kwa nafasi ya urais, taarifa za walio na kusudio la kugombea nafasi hiyo zitawasilishwa kwa Katibu Mkuu na kujadiliwa na Kamati Kuu na kutolewa uamuzi."

Kwa mujibu wa Mnyika, kifungu hicho cha mwongozo kinaeleza kuwa baada ya taarifa za watia nia kujadiliwa na Kamati Kuu, zitatolewa uamuzi kwa hatua nyingine.

Alisema kwa mujibu wa chama hicho, kutia nia ya urais ni mchakato wa ndani wa chama ambao utafuatiwa na hatua nyingine ambazo hawatazitangaza mpaka taratibu za hatua hiyo ya awali zitakapokamilika.

"Taratibu nyingine zitakazofuata tutatangaza baadaye wakati muafaka, ambazo ni ratiba ya uchaguzi yenye kuhusisha tarehe ya kuchukua na kurudisha fomu, taratibu za wagombea urais kutafuta wadhamini, vikao vya uteuzi na mchakato mzima wa uteuzi ambao unaanzia kwenye Kamati Kuu ya chama ambayo imepewa mamlaka ya kikatiba ya kutafiti jina la mgombea urais, mchakato unaokwenda mpaka kwenye baraza kuu," alisema Mnyika.

Alisema uamuzi huo wa kufungua mlango wa watia nia ya urais haujafunga mlango wa majadiliano na vyama vingine vyenye nia ya kweli ya kuondoa CCM madarakani katika kuelekea uchaguzi mkuu.

"Tutakuwa tukiwaeleza kwa kadiri ya mazungumzo na vyama ambavyo kwa dhati vimeonyesha dhamira kwa majadiliano," alisema Mnyika.

Alisema majadiliano ya ushirikiano huo waliyofungua ni ya ngazi zote kuanzia udiwani, uwakilishi, ubunge, urais wa Zanzibar na urais wa Jamhuri ya Muungano.

"Tutakapokaa na wenzetu ambao tumefungua milango ya majadiliano watakapokuwa tayari, tutaona namna ya ushirikiano inayofaa katika mazingira ya sasa, lakini dhamira yetu ni ushirikiano wa pamoja kwa vyama vyenye nia ya kweli na dhati katika kuiondoa CCM madarakani," alisisitiza Mnyika.

Akizungumzia kuhusu waliotangaza nia kabla ya kutolewa kwa tangazo na chama hicho, Mnyika alisema chama hicho kitatambua watia nia ambao watakuwa wamewasilisha barua ya nia yao hiyo kwa Katibu Mkuu kuanzia tangazo hilo lilipotolewa.

Kuhusu ratiba ya watia nia kwa nafasi za ubunge na udiwani, Mnyika alisema hiyo itatangazwa katika hatua nyingine itakayofuata.

Pia, Mnyika alisema katika kipindi kifupi kilichobaki kabla ya kuvunjwa kwa bunge, bado chama hicho kitaendelea kudai Tume huru ya uchaguzi.

"Kwa dakika zilizobaki za lala salama, kwa ratiba iliyotolewa na Bunge, kuna mwanya umebaki finyu sana wa kati ya Juni 5 na 10 ambapo bunge bado linashughulikia miswada na hoja mbalimbali. Kuna ka mwanya kadogo bado kamebaki kuendelea kudai tume huru ya uchaguzi," alisema Mnyika.

"Tunaendelea kutoa rai kwa Rais na Bunge kwamba kwa huu mwanya uliobaki, upelekwe bungeni mswada wa marekebisho ya sheria utakaowezesha kuwe na tume huru ya uchaguzi," aliongeza Mnyika.

CHATAMBA KUIONDOA CCM

Alisema chama hicho kimejiandaa kwa mikakati ya namna nyingine ya kuhakikisha wanaiondoa CCM madarakani katika sanduku la kura.

"Kwa mikakati tutakayoitumia na kwa chochote kitakachotokea, watawala watabeba mzigo wa lawama," alisema Mnyika.

Kwa mujibu wa katibu huyo, Katiba ya nchi ibara ya 8 inasema madaraka na mamlaka ni ya wananchi.

"Katika wakati mwafaka tutawaongoza wananchi kutumia madaraka na mamlaka yao kufanya mabadiliko katika taifa hili, kwa hiyo tunadai tume huru ya uchaguzi na tutaendelea kuidai, lakini hatuwezi kuacha kujiandaa kwa harakati na kazi ya kuiondoa CCM madarakani, tukisubiri siku watakayoileta," alisema Mnyika.

## Mbaroni mauaji ya dereva teksi

**Na Romana Mallya**

WATU watatu wanashikiliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Kinondoni, kwa tuhuma za kumuua dereva teksi, Joseph Mwenda na kumzika maeneo karibu na Shule ya St. Mary's, Mbezi Makonde jijini Dar es Salaam kisha kuondoka na gari.

Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Edward Bukombe, alithibitisha kutokea kwa mauaji hayo yanayodaiwa kufanywa na watu hao watatu Mei 21, mwaka huu.

Kamanda Bukombe alilitaja gari ambalo liliibiwa baada ya mauaji hayo kuwa ni lenye namba za usajili T 139 DST aina ya IST.

"Huyu dereva alitoweka kuanzia Mei 21, hakurudi nyumbani, mwenye gari akamtafuta mwishoe akatoa taarifa polisi na ufuatiliaji ulianza mara moja, lakini tulipoipiga namba ya simu ya huyu dereva ilikuwa haipatikani.

"Maongezi ya mwisho yalionyesha aliongea na nani ndipo tukaanza kuwafuatilia na kufanikiwa kuwakamata watu wawili na mwingine wa tatu alikamatwa baadaye, na walipohojiwa walikiri wao ndiyo waliomteka, kumuua na kumfukia kisha wakaiba gari."

Alisema watu hao waliwapeleka polisi eneo ambalo walimfukia dereva huyo maeneo ya Mbezi Juu na juzi na kuonyesha gari waliloliiba.

Mmiliki wa gari hilo ambalo limeunganishwa na mfumo wa bolt zamani taxify, Emmanuel Flavian, akizungumza Nipashe, alisema Joseph alizikwa jana maeneo ya Mbezi kwa Msuguli, jijini Dar es Salaam.

Baada ya tukio hilo la kupotea kwa dereva huyo pamoja na gari, mmiliki wa gari hilo alisambaza picha ya dereva, gari na taarifa ya Mei 22 ya kupotea kwake aliyoitoa polisi ambayo ni KMT/RB/12351.

Mmoja wa madereva akisimulia tukio hilo baada ya kujirekodi na kutupia mtandaoni bila kutaja jina lake, alidai marehemu ambaye alikuwa akiendesha gari hilo lililounganishwa na mfumo wa taxify alikodiwa na watu kutoka Posta kwenda Mbezi Juu.

"Meneja wa taxify alitoa ushirikiano mzuri kwa ndugu wa merehemu na polisi na kutoka namba ya mtu ambaye alimkodi siku hiyo mara ya mwisho kwa sababu alitumia namba ya taxify ndipo akafuatiliwa na kukamatwa na kukutwa na simu ya marehemu nyumbani kwake.

"Hizi kazi zetu tumuombe sana Mungu, hujui ni wapi utapata matatizo au shida kwa sababu halikuwa muda wa saa 12 wala siyo usiku dereva huyu alikodiwa, tumuombe sana Mungu, binadamu wamekuwa wanyama," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Tanzania yasitisha shughuli mpaka Namanga

**Na Daniel Sabuni, NAMANGA**

MPAKA wa Namanga upande wa Tanzania umesitisha shughuli zote za kibiashara na nchi jirani ya Kenya kwa muda kutokana na nchi hiyo kutoamini vyeti vya ugonjwa wa Covid -19 unaosababishwa na virusi vya corona vya madereva wa malori wa Tanzania vinavyoonyesha kuwa hawajaambukizwa.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, ameiambia Nipashe jana kuwa hatua hiyo imefikiwa baada ya upande wa Kenya kukiuka makubaliano ya pande hizo mbili, waliyotiliana saini Mei, mwaka huu kwa kuzuia madereva wa Tanzania, kukataa vyeti ili wawaruhusu kuingia Kenya.

"Nadhani wenzetu wana ajenda ya siri kutuhujumu kiuchumi, tumeshakubaliana dereva anapopimwa upande wa Tanzania aruhusiwe upande wa Kenya kwa cheti, sasa wamekiuka makubaliano, wakifika upande ule wanataka wawapime tena sijui wana maana ipi nashindwa kuwaelewa kabisa, tumeamua kuchukua hatua na haturudi nyuma," alisema.

Katika makubaliano hayo waliamua katika lori itaruhusiwa dereva na wasaidizi wawili kuingia katika nchi husika wote wakiwa wamepimwa kama wana maambukizo ya corona.

Hata hivyo, alisema upande wa Kenya wamebadilika juzi (Jumatatu) kwa kuzuia na kutaka kuwapima tena.

"Pamoja na juhudi za mimi na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, kuwasiliana na viongozi wenzetu wa Kenya, lakini zimegonga mwamba na ndipo tukaamua kuzuia vyeti vyote na magari ya mizigo kutoka Kenya pamoja bidhaa zote zinazoingia kutoka nchini humo hadi hapo tutakapokaa tena na kufikia muafaka maana sote tunategemeana, Kenya wanatuhitaji kama soko na sisi wanatuhitaji pia ili kuuza bidhaa," alisema Mwaisumbe.

Alisema mwezi Mei makubaliano ya kuruhusu kuaminiana pande mbili yalikaliwa kikao na mawaziri wa mambo ya nje za nchi, makatibu wakuu, wataalamu na viongozi wengine wa mikoa na wilaya wa kutoka nchi mbili katika mpaka wa Namanga, kufuatia mazungumzo ya Rais John Magufuli na Rais Uhuru Kenyata ambao waliwaagiza viongozi wanaohusika kukaa na kufanya vikao na makubaliano, huku wakichukua tahadhari za ugonjwa huo na kuona namna ya kuendelea na biashara kwa nchi hizo.

Alisema kama hali ya kutoaminiana itaendelea, itawalazimu kutoa uamuzi wa kuigeuza Namanga kuwa bandari kavu na majirani Wakenya watashusha mizigo au bidhaa upande wake na Tanzania kuichukua na pia hata Tanzania itapeleka wa Tanzania ili Kenya waifuate.

"Nchi yetu ni huru inayojitegemea haihitaji kubembeleza nchi nyingine kufanya biashara kwa sababu sisi tunategemeana, haiwezekani mambo ambayo yameagizwa na marais viongozi wa chini hawatekelezi... linaashiria dharau na ajenda ambayo wanadhani ni siri iliyofichika kumbe sisi tunaifahamu, hatutaweza kuivumilia hata kidogo," alisema.

Alisema, nia ya Rais Magufuli ni kuwasaidia watu wa hali ya chini kwa kuwa uamuzi huo unapofanyika wanao umia ni watu wa chini.

"Nataka nikuhakikishie ndugu kupima kipimo cha Covid-19 sio lelemama kinaumiza sana, sasa haiwezekani siku mbili mtu amechokonolewa pua, halafu anatoka upande wa Tanzania anaenda upande wa Kenya anafanyiwa kitu kile kile, sasa hali hii kwa kweli sio sahihi, tunataka hiyo agenda yao ya siri ijitokeze hadharani tushughulike nayo kuliko kutumia ugonjwa wa Covid-19, sisi hatutakuwa tayari," alisema Mwaisumbe.




Diwani wa Kata ya Kilimanjaro Manispaa ya Moshi, Priscus Tarimo (kushoto), akikabidhi sehemu ya mapipa ya maji kwa ajili ya kunawia mikono kwa shule za sekondari za manispaa hiyo, mkoani Kilimanjaro jana, yaliyotolewa na kampuni ya vinywaji baridi ya IPP-Bonite Bottlers, ili kuwasaidia wanafunzi wa kidato cha sita, kujikinga na maambukizo ya corona. Shule za sekondari zilizonufaika ni Mawenzi, Moshi na Moshi Technical. **PICHA: JAMES LANKA**

# Mahakama yatupilia mbali kesi dhidi ya Spika, AG, mbunge

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu, Kanda ya Dar es Salaam, imetupiliwa mbali kesi ya Kikatiba dhidi ya Spika wa Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Job Ndugai na wenzake kwamba imefunguliwa kinyume na utaratibu.

Kesi hiyo ilifunguliwa na Wakili Paul Kaunda dhidi ya Spika Ndugai, Mbunge wa Jimbo la Ndanda kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), ambaye kwa sasa amehamia CCM, Cecil Mwambe na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Mahakama hiyo iliyoketi chini ya jopo la majaji watatu likiongozwa na Mwenyekiti, Issa Maige, akisaidiana na Stephen Magoiga na Seif Kulita, ilitoa uamuzi huo baada ya kusikiliza pingamizi la awali lililowasilishwa na Mwanasheria Mkuu.

Jaji Maige alisema jopo wamekubaliana na hoja za Mwanasheria Mkuu kwamba mlalamikaji amekosea kufungua kesi hiyo kwa kutumia ibara ya 26, bali alipaswa ajiegemeza katika ibara ya 83 ya Katiba ikiwa sambamba na kifungu cha 37 cha Sheria ya Uchaguzi.

Ibara hiyo inaelekeza utaratibu wa kuwasilisha malalamiko kama yaliyowasilishwa na mlalamikaji.

Alisema maneno aliyotamka Spika yako katika msingi na utaratibu wa kawaida katika utendaji wake.

Katika kesi ya msingi, Wakili Kaunda anadai Mwambe alitangaza kujivua uanachama wa Chadema na kujiunga na CCM kauli ambayo iliungwa mkono na Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, aliyempokea rasmi Mwambe mbele ya hadhira kwa kumkabidhi kadi ya CCM, na Mwambe naye alimkabidhi Katibu Mkuu huyo kadi yake ya Chadema.

Wakili Kaunda anadai kitendo cha Spika kumtambua Mwambe kama Mbunge halali wakati ameshajivua uanachama wa chama kilichomdhamini kama Mbunge wa Ndanda (2015-2020), ni ukiukwaji wa ibara ya 71(1)(f) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na hakuna mamlaka yoyote nchini, achilia mbali Spika, yenye uwezo wa kumrudisha bungeni mbunge ambaye kwa hiyari yake mwenyewe ameamua kujivua uanachama wa chama cha siasa kilichomdhamini kupata ubunge.

Katika hoja za awali za serikali, pamoja na mambo mengine ilidai kuwa shauri hilo halistahili kwa kuwa linakinzana na Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu wa Msingi, pamoja na Ibara ya 26(2) ya Katiba ya nchi.

Pamoja na pingamizi hilo pia serikali katika majibu yake inadai kuwa Mwambe bado ni Mbunge halali wa Ndanda kwa mujibu wa Katiba na sheria nyingine za nchi na anastahili stahiki zote kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazotumika kusimamia masuala ya Bunge.

Serikali inadai kuwa Spika hajavunja sharti lolote la Katiba ya nchi kama inavyodaiwa, na hivyo inamtaka mdai kuthibitisha madai yake.


**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**President's Office – State House**
**TANZANIA SOCIAL ACTION FUND**

**INVITATION FOR QUOTATIONS**
**FOR**
**TZ-TASAF-166381-GO-RFQ TO SUPPLY NETWORK EQUIPMENT**

**TZ-TASAF-166384-GO-RFQ TO SUPPLY VIDEO CONFERENCE SOLUTION AND TELEPHONE HANDSETS**

**Date: 1st June, 2020**

1. The United Republic of Tanzania has received financing from the World Bank and support from United States Agency for International Development (USAID), Bill and Melinda Gates Foundation, The Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis & Malaria International Fund for Agriculture Development, the NORWAY Government and OPEC FUND towards the cost of the Productive Social Safety Net Project II.

2. You are hereby invited to submit your price quotation for supplying Network Equipment and Telephone Handsets as described in the Schedule of Requirements and Prices attached in Section II of the Invitation for Quotations document.

3. The Invitation for Quotations document is available in the TASAF Website www.tasaf.go.tz for interested bidders where also amendment or clarifications for the same will be posted.

4. All quotations, properly filled in, addressed to: The Executive Director, Tanzania Social Action Fund, 4th Floor, PSSSF Plaza, Jakaya Mrisho Kikwete Road, P. O. Box 2719, Dodoma, Tanzania shall be submitted via e-mail. Electronic Bidding will not be permitted except e-mail submission as detailed in ITT 17 in view of COVID-19. Quotations shall be valid for 45 days.

5. The required delivery period is 60 days from the date of local purchase order.

6. Deadline for submission will be on 17th June, 2020 at 10:00 hours local time. Quotations will be opened promptly thereafter through live stream in YouTube in the following link https://youtu.be/uWLwuQQ7JFE and the opening event will be recorded and posted on the TASAF's website www.tasaf.go.tz for viewing in view of COVID-19.

7. Late quotations, portion of quotations, quotations not received, quotations not opened at the quotation opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**The Executive Director,**
**Tanzania Social Action Fund,**
**4th Floor, Board of Trustees of Public Service Social Security Fund Building,**
**Jakaya Mrisho Kikwete Road,**
**P. O. Box 2719,**
**Dodoma, Tanzania**

HABARI KITAIFA

# JPM, Shein wakutana kikao cha ndani Dodoma

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. John Magufuli na Mwenyekiti wa CCM Taifa, jana amekutana na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, katika kikao cha ndani kilichofanyika Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma.

Taarifa iliyotolewa na Ikulu Chamwino, ilisema kikao hicho kimehudhuriwa na Makamu Mwenyekiti CCM Bara, Philip Mangula na Katibu Mkuu wa chama hicho, Bashiru Ally, kuzungumzia masuala ya chama hicho.

Taarifa hiyo ilisema, baada ya kikao hicho, Rais Shein alikwenda kuweka udongo katika jiwe la msingi la ujenzi wa Ofisi za Ikulu na kukagua maendeleo ya kazi ya ujenzi wa ofisi hizo inayofanywa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kupitia shirika lake la Suma JKT.

Rais Shein alimshukuru Rais Magufuli kwa kumpa fursa ya kwenda kuweka udongo ikiwa ni kumbukumbu ya ujenzi wa ofisi hizo na kubainisha kuwa kujengwa kwa ofisi hiyo ni heshima kwa taifa na tafsiri sahihi ya kujitawala.

"Huko ndio kujitawala, kutawaliwa sio kuzuri, mtawala anafanya anavyotaka yeye, anafanya kwa utashi wake pale anapotaka yeye kufanya, tunapochukua hatua ya kujitawala wenyewe tunafanya mambo makubwa kama haya kwa ajili ya wananchi, hii ofisi ni ya wananchi wa Tanzania," alisema Rais Shein.



Meneja wa Kiwanda cha Tanzania Distillers Ltd (TDL), Aranyaeli Ayo (kulia) akitoa maelezo ya shughuli za kiwanda kwa ujumbe wa maofisa waandamizi kutoka taasisi za serikali za TANTRADE, TIRDO na BRELA, waliofanya ziara ya kikazi kiwandani hapo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtoto atuhumiwa kumuua mama kwa kumkaba shingo

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

JUSTINE Joseph, mkazi wa Kijiji cha Omungando, wilaya ya Kyerwa mkoani Kagera, anatuhumiwa kumuua mama yake mzazi, Theopista Joseph (72), kwa kumshambulia kwa kipigo na kumkaba shingo hadi kufa.

Kamanda wa Polisi mkoani hapo, Revocatus Malimi, amethibitisha tukio hilo la mauaji kuwa, Mei 5, mwaka huu saa tatu usiku, mtuhumiwa alimvamia mama yake akiwa njiani kurudi nyumbani na kuanza kumgombeza kwa kutomhudumia mgonjwa nyumbani.

Malimi alisema polisi ilifanya uchunguzi wa awali baada ya mtuhumiwa kukimbia kusikojulikana na kubaini kuwa baba wa familia hiyo, ambaye ni baba mzazi wa mtuhumiwa aliugua kwa kipindi kirefu ugonjwa wa kiharusi.

Alisema, mkewe (marehemu) anadaiwa kutomuuguza vizuri mume wake, badala yake alimuacha ndani na kwenda kunywa pombe vilabuni licha ya kushauriwa na mtuhumiwa asiende kunywa.

"Marehemu alishauriwa na mtuhumiwa ambaye ni mwanawe kwamba asiende kunywa pombe jambo lililokuwa likimpa hasira, kwa sababu ya kutokaa nyumbani kumpatia huduma baba yake," alisema Malimi.

Katika tukio lingine Kamanda Malimi alisema Juni mosi, majira ya saa tatu usiku kijijini Igabilo, wilayani Muleba, yalitokea mauaji ya Happiness Ibrahim (33), yaliyosababishwa na kipigo cha mume wake, Hamis Luge (36).

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni kutoelewana na mume wake aliyemtaka kuacha kunywa pombe na kurudi nyumbani ili yeye aende kuvua samaki mwaloni.

"Kwa uchunguzi wa awali mtuhumiwa aliacha amemzuia mke wake asiendelee kunywa pombe, lakini mke alikaidi na kuendelea kunywa hadi mume wake aliporudi saa 2:00 usiku na kumkuta bado yuko kilabuni," alisema Malimi.

Alisema mtuhumiwa alimfuata mkewe kilabuni na kumtaka waondoke kurudi nyumbani, lakini mke aligoma.

Kamanda aliendelea kueleza kuwa mtuhumiwa alimchukua kwa nguvu mkewe badi nyumbani na kuanza kumpiga hadi kumsababishia kifo baada ya kuzidiwa na kipigo ambacho kilisababisha majeraha kichwani.

# Muuguzi kortini madai kuomba rushwa 60,000/- kusafisha kizazi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MUUGUZI wa Zahanati ya Chamwino Jijini Dodoma, Richard Zablon (32), amefikishwa mahakamani kwa tuhuma za kupokea rushwa ya Sh. 60,000 ili kutoa huduma ya kumsafisha kizazi mgonjwa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(Takukuru), Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema mshtakiwa huyo alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma, na kufunguliwa shauri la jinai namba 13/2020 mbele ya Hakimu Paschal Mayumba.

Alisema mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani hapo kwa kuomba rushwa ya Sh.100, 000 na kupokea Sh. 60,000 kinyume cha kifungu cha 15(1)(a)cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 marejeo ya mwaka 2019.

"Mei 11, mwaka huu tulipokea taarifa kutoka kwa mwananchi mmoja kwamba mkewe yupo katika Zahanati ya Chamwino akihitaji huduma ya kusafishwa kizazi, lakini mshtakiwa amehitaji apatiwe fedha ndipo afanye kazi hiyo,"alisema.

Kibwengo alisema wakati mtoa taarifa bado yupo ofisini kwao, mshtakiwa huyo alimpigia simu akisisitiza apewe fedha yake kwa kuwa tayari ameshamsafisha mgonjwa.

"Lakini akaelezwa kwamba amwache mgonjwa aondoke kwani fedha zake atapelekewa, hata hivyo mshtakiwa aligoma na kuamua kuondoka na mgonjwa kwenye gari yake binafsi kwenda naye nyumbani kwa mgonjwa ili akapewe fedha," alisema.

Alisema maofisa wa taasisi hiyo walimkamata mtuhumiwa huyo na baada ya kukamilisha uchunguzi wakamfikisha mahakamani.

Wakati huo huo, Taasisi hiyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Mashtaka ya Mkoa wa Dodoma, inatarajiwa kumfikisha katika Mahakama ya Wilaya ya Bahi Yusufu Chuma (39), Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mpamatwa kwa tuhuma za kughushi nyaraka.

Mkuu huyo alisema mwalimu huyo anakabiliwa na makosa manne ya kugushi na kuwasilisha nyaraka zenye maelekezo ya uongo kinyume ca Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 Marejeo ya mwaka 2002.

"Uchunguzi wetu umeonyesha Juni mwaka 2019 mtuhumiwa aligudhi mihtasari miwili ya vikao vya Kamati ya Shule na Mkutano wa walimu kuonyesha kwamba waliridhia kiasi cha Sh.469, 500 kitolewe kwenye akaunti ya shule na kuwasilisha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kuomba ridhaa yake," alisema.

Alisisitiza kuwa fedha katika ngazi za shule hutolewa benki baada ya vikao halali kwa kuridhia ili kujua matumizi ya fedha hizo na kudhibiti ufujaji pamoja na kuboresha uwajibikaji.

# Vyuo vyapewa saa 48 kulipa wanafunzi

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, ametoa saa 48 kwa vyuo vikuu nchini kuhakikisha wanafunzi wote wamepewa fedha zao za kujikimu.

Amesema chuo chochote ambacho kitakuwa hakijatekeleza agizo hilo hakitakuwa na msamaha zaidi ya kukichukulia hatua.

Alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam wakati akikabidhi magari manne yenye thamani ya Sh. milioni 700 kwa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), yaliyonunuliwa na serikali kupitia mkopo wa Benki ya Dunia (WB) uliotolewa kwa ajili ya uboreshaji wa sekta ya elimu nchini.

"Ifikapo Ijumaa wanafunzi wote wa vyuo vikuu wawe wameshapata fedha zao zote za kujikimu, kwa sababu serikali imeshatoa Sh. bilioni 122 kwa ajili yao sasa kwa nini wacheleweshewe? Hakutakuwa na msamaha kwa vyuo ambavyo vitakuwa havijatekeleza agizo hilo," alisema Prof. Ndalichako na kuongeza:

"Rais Magufuli alishatoa maelekezo na lazima yatekelezwe. Sasa ole wao vyuo vitakavyokuwa havijatekeleza agizo hilo, kama kutakuwa na wanafunzi ambao watakuwa hawajasaini fedha za kujikimu achaneni nao wapeni ambao wameshasaini."

Prof. Ndalichako alisema ni uamuzi unaolenga kutekeleza agizo la Rais John Magufuli alilolitoa hivi karibuni kwa kuvitaka vyuo vikuu kukamilisha mchakato huo haraka kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi kusoma bila changamoto wakati huu ambao wanakabiliwa na ufinyu wa muda kutokana na ratiba ya masomo kusimama kutokana na ugonjwa wa corona.

"Najua wanafunzi wengi kwa sasa wamesharejea vyuoni kuendelea na masomo yao na kama alivyoagiza Rais Magufuli fedha za mikopo kwa ajili ya wanafunzi hawa wanapaswa kupewa haraka, nami kwa nafasi hiyo naviagiza vyuo vyote kuhakikisha hadi Ijumaa wanafunzi wawe wamepewa fedha zao, chuo kitakachoshindwa kutekeleza hilo hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya watakaohusika," alisema Prof. Ndalichako.

Alisema ni muhimu kwa agizo hilo kutekelezwa kwa wakati bila ya kuwapo kwa visingizio kutoka katika vyuo hivyo kwa kuwa tayari wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), ilishajihakikishia kuwa mipango ya utoaji wa fedha hizo upo tayari na kwamba kilichokuwa kikisubiriwa ni mchakato wa vyuo hivyo pamoja na wanafunzi kurejea vyuoni.

"Sitopenda kusikia sababu yoyote hata kama ikionekana kuna mwanafunzi anazembea mwenyewe kujisajili mnaachana naye na kuendelea na wengine, nalisisitiza hili ili kuwakumbusha wahusika wote mtekeleze wajibu wenu ipasavyo," alisema.

Aidha, Prof. Ndalichako alipongeza NIT kwa kupiga hatua kubwa za kimaendeleo suala inalokisaidia kwenda na mipango mikakati ya serikali ya kuzalisha wataalamu mbalimbali katika sekta ya anga na usafirishaji, hivyo kutoa fursa ya nguvu kazi katika miradi mbalimbali ya serikali.


**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**President's Office – State House**
**TANZANIA SOCIAL ACTION FUND**

## RE-INVITATION FOR QUOTATIONS FOR SUPPLY SUNDRY ITEMS

**Date: 1st June, 2020**

1. The United Republic of Tanzania has received financing from the World Bank and support from United States Agency for International Development (USAID), Bill and Melinda Gates Foundation, The Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis & Malaria International Fund for Agriculture Development, the NORWAY Government and OPEC FUND towards the cost of the Productive Social Safety Net Project II.
2. You are hereby invited to submit your price quotation for supplying sundry items as described in the Schedule of Requirements and Prices attached in Section II of the Invitation for Quotations document.
3. The Invitation for Quotations document is available in the TASAF Website www.tasaf.go.tz for interested bidders where also amendment or clarifications for the same will be posted.
4. All quotations, properly filled in, password protected must be delivered to the following email address in electronic format: **miriam.malyeta@tasaf.go.tz.**
5. The Quotations shall be valid for 45 days
6. The required delivery period is 7 days from the issuance of the purchase order.
7. Deadline for submission will be on 16th June, 2020 at 10:00 hours local time. Quotations will be opened promptly thereafter through live stream in YouTube in the following link **https://youtu.be/F45aXQ_c69U** and the opening event will be recorded and posted on the TASAF's website **www.tasaf.go.tz** for viewing in response to to COVID-19 . Submission and opening details are provided in ITB Clause 17.
8. Late quotations, portion of quotations, quotations not received, quotations not opened at the quotation opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

Electronic Quotation will not be permitted except e-mail submission as detailed in ITB Clause 17.

**The Executive Director,**
**Tanzania Social Action Fund,**
**4th Floor, Board of Trustees of Public Service Social Security Fund Building,**
**Jakaya Mrisho Kikwete Road,**
**Dodoma, Tanzania**



**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**President's Office – State House**
**TANZANIA SOCIAL ACTION FUND**

## QUOTATION No: TZ-TASAF-161710-NC-RFQ for CAR HIRE SERVICES

## RE-INVITATION FOR QUOTATIONS

Date: 1st June, 2020

1. This Invitation for Quotation (IFQ) follows the General Procurement Notice for this Project which appeared in UN Development Business Issue no. WB-P475857-02/20 dated 4th February, 2020.
2. The Government of the United Republic of Tanzania has received financing from the World Bank toward the cost of the Productive Social Safety Net II. This project will be jointly financed by the Agency for International Development, Bill and Melinda Gates Foundation, The Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis & Malaria, International Fund for Agriculture Development, The government of NORWAY and OPEC. The Tanzania Social Action Fund (TASAF) Management Unit, the implementing agency for this Project intends to apply part of the proceeds to cover eligible payments under the contract for which this IFQ is issued.
3. You are hereby invited to submit your priced quotation for the provision of the services as described in the Statement of Requirement (SoR) and Prices as detailed in Section II. The Invitation for Quotations document is available in the TASAF Website www.tasaf.go.tz for interested bidders where also amendment or clarifications for the same will be posted.
4. All quotations, properly filled in, password protected must be delivered to the following email address in electronic format: **miriam.malyeta@tasaf.go.tz.**
5. Deadline for submission will be on **16th June, 2020 at 10:00 hours local time**. Quotations will be opened promptly thereafter through live stream in YouTube in the following link https://youtu.be/99Kj3Tyad4s and the opening event will be recorded and posted on the TASAF's website www.tasaf.go.tz for in response to COVID-19 .. Submission and opening details are provided in ITB Clause 17
6. Late, partial, and quotations not read at the quotation opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

Electronic Quotation will not be permitted except e-mail submission as detailed in ITB Clause 17

**The Executive Director,**
**Tanzania Social Action Fund,**
**4th Floor, Board of Trustees of Public Service Social Security Fund Building,**
**Jakaya Mrisho Kikwete Road,**
**P. O. Box 2719,**
**Dodoma, Tanzania**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Shida hizi sasa zimalizwe vijijini

MOJA ya taarifa zetu za leo ni kilio cha wakazi wa Kijiji cha Madundasi katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, kulalamikia kulipishwa Sh. 400,000 kupeleka mgonjwa hospitalini.

Wanatozwa fedha hizo kwenye bodaboda wakitaka kupeleka wagonjwa Hospitali ya Wilaya ya Chunya kutokana na barabara kutopitika.

Wananchi hao wanalazimika kulipa nusu milioni kutokana na barabara zinazounganisha kijiji hicho kujaa maji hivyo kutopitika.

Viongozi wa kijiji wanasema tatizo la barabara ni kubwa kijiji cha Madundasi, zipo taarifa za vifo na wananchi wengi wanaendelea kupoteza maisha kutokana na ubovu wa barabara hizo.

Ni wazi kuwa taarifa hizo zimewafikia viongozi na wadau katika kipindi hiki cha bajeti na zinakuwa kama kengele ya kuwaamsha kufanyakazi zaidi.

Kwa serikali kinachotakiwa ni kasi zaidi ya kutekeleza ahadi na kuhakikisha kuwa kila kijiji kinapata huduma za afya pamoja na miundombinu inayopitika wakati wote.

Miundombinu hiyo ni mahususi kusafirisha mazao ya wakulima na kufikisha wagonjwa na wazazi hospitalini kwa wakati.

Kinachotokea Madundasi si kigeni. Huenda vijiji vingi vina shida hiyo pengine havina hospitali au wahudumu wa afya au dawa na huduma za rufani.

Hali hiyo huwalazimisha wagonjwa au familia zao kuelekea kwenye huduma za rufani na tatizo linalojiri ni ubovu wa barabara.

Tunafahamu kuwa serikali imeanzisha Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) ili kukabili changamoto za ubovu wa miundombinu kwenye ngazi za halmashauri na vijijini.

Kwa hiyo tunashauri manispaa na wilaya zikishirikiana na Tarura, kuangalia changamoto za kiafya vijiji na kutafuta njia bora zaidi za kuwasaidia wagonjwa ambao pengine si wengi wanaoweza kumudu gharama za Sh. 400,000 kwa mara moja kupeleka mgonjwa hospitali.

Aidha, tunapenda kusema kuwa ukosefu wa barabara na huduma za afya unawaathiri zaidi kinamama na watoto iwe kwa wajawazito, wazazi au wazazi na watoto wachanga.

Tunashauri kuwa ni vyema vijiji vyenye changamoto za huduma za afya na miundombinu mibovu vikatambuliwa na kupewa kipaumbele.

Tunaamini jicho la Tarura likiwa kwenye vijiji hivyo itasaidia kupunguza changamoto, lakini halmashauri zikifahamu kuhusu vijiji vyenye changamoto kubwa za matibabu ni rahisi pia kuandaa mbinu za kukabiliana na changamoto za wagonjwa.

Tatizo la ukosefu wa zahanati na barabara ni chanzo cha vifo vya wanawake vinavyotokana na uzazi.

Aidha, ukosefu unahusika pia na vifo kwa watoto wachanga au wadogo hivyo si suala la kulikalia kimya ni muda wa kuangalia namna bora ya kutatua changamoto hiyo.

Halikadhalika, tunaiomba serikali kuangalia changamoto hiyo hasa kipindi hiki ambacho bajeti inatarajiwa kusomwa jijini Dodoma.

Licha ya ahadi ya kujenga zahanati kwa kila kijiji na nyumba ya mkunga na ya daktari na kituo cha afya kwa kila kata, Tarura nayo ihakikishe kuwa huduma hizo zinafikika hasa wakati wa mvua.

Tunakishauri chombo hicho kuangalia njia bora za muda za kuunganisha zahanati vijijini na vituo vya afya ili kuokoa maisha ya watu.

Tunaamini wabunge watalifuatilia hilo na kuelekeza namna bora ya kutatua matatizo hayo ambayo ni kama changamoto za muda mrefu zinazowatatiza wananchi wetu hasa wa vijijini.

Tunaamini kuwa hakuna jambo geni kwa vile taasisi za kushughulikia matatizo ya wananchi zina taarifa zote kuanzia madaraja, mabovu, barabara zisizopatikana na maeneo yasiyo na hospitali, zahanati wala vituo vya afya.

Ni wito wetu kuwa kwa vile azma ya serikali ni kuwahudumia wananchi basi mamlaka za utekelezaji zisizembee.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hofu yaweza kukwamisha vita dhidi ya virusi vya corona

Na Sabato Kasika

KABLA na hata baada ya kuingia kwa ugonjwa wa corona nchini, jitihada zimekuwa zikifanywa na serikali na wadau wa afya. Hapo kuna kuelimishana, kujua mbinu mbalimbali za kujikinga na ugonjwa huo.

Umma unaendelea kuelekezwa namna ya kujikinga uvaaji barakoa, kunawa mikono kwa maji tiririka, kupaka vitakasa mikono, kutosalimiana kwa kushikana mikono, kukumbatiana na pia kutokaribiana.

Magari ya abiria sasa yanabeba kulingana na idadi ya viti, hakuna msongamano, lengo kuhakikisha usalama wa Watanzania, dhidi ya ugonjwa huo unaoendelea kutikisa dunia.

Hata hivyo, kuna sintofahamu itokanayo na baadhi ya watu kujawa hofu, wengine wanashindwa kwenda kwenye shughuli zao za kila siku.

Wanafanya hivyo, huku wakiwa tayari wameshaelekezwa jinsi ya kujikinga na kuendelea na shughuli zao za kila siku, ratiba zao ziongozwe na umakini wa kulinda afya zao kwa kuzingatia maelekezo waliopewa.

Hofu hiyo, ilishamuibua hata Rais Dk. John Magufuli hivi karibuni, alipowakumbusha Watanzania watulie na kuwajibikia yaliyo mbele zao.

Katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu, kuna ufafanuzi wa neno hofu, kwamba "ni hali ya kutokuwa na ushujaa, woga, jambo linaloleta woga au kitisho, shindwa kukabili jambo lihitajilo vikumbo, kuwa na woga, ogopa, chelea na hatihati."

Hayo yote ndiyo yanatokana na hofu hadi watu kusahau maelekezo ya kitaifa na kitaalamu kuhusu kujikinga, hata shughuli za uzalishaji mali zinakwama.

Kwa maana hofu haina nafasi tena. Kwani tikizingatia, haya hofu isipewe nafasi, kwa kuwa nao ni ugonjwa mwingine ambao ukiendelea kupewa nafasi unaweza kusababisha mengine, binadamu anaposhindwa kwa sababu ya hofu, hukata tamaa.

Iwapo kutakuwapo kukata tamaa, maana yake ni kuacha maelekezo ya wataalamu wa afya na hivyo kuruhusu ugonjwa huo kuendelea kuchukua nafasi badala ya kuukabili na kuutokomeza.

Ni kweli kila mtu ameumbwa na hofu ndani ya moyo wake, ambayo humsaidia pengine kuepuka vitu hatarishi katika maisha, na hilo haliepukiki katika maisha ya binadamu.

Ukweli ni kwamba kila siku mtu anapatwa na hofu juu ya mambo mbalimbali, kwani ni jambo la kawaida katika maisha ya mwanadamu, lakini pia imekuwa kikwazo cha mafanikio kwa baadhi ya watu katika maeneo mbalimbali.

Ikumbukwe kuwa, hofu hujenga uoga ndani ya mtu na kumfanya ashindwe kuchukua hatua juu ya jambo husika, na ni kikwazo katika mafanikio, hivyo ikiendelea kupewa nafasi, inaweza kukwamisha vita ya virusi vya corona.

**Wanafanya hivyo, huku wakiwa tayari wameshaelekezwa jinsi ya kujikinga na kuendelea na shughuli zao za kila siku, ratiba zao ziongozwe na umakini wa kulinda afya zao kwa kuzingatia maelekezo waliopewa.**

Hivyo, wakati huu wa vita dhidi ya virusi vya corona, siyo wa kuweka hofu mbele, badala yake iwekwe pembeni na kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya kama ambavyo rais amekuwa akisisitiza.

Watanzania pia wanashauriwa kutumia njia za asili za kupambana na ugonjwa huo ikiwamo ya kujifukiza, huku Wizara ya Afya ikiagizwa kufafanua ni namna gani suala la kujifukiza linasaidia kudhibiti corona.

Maana yake ni kwamba kila mmoja ajitahidi kadri inavyowezekana kujikinga na ugonjwa huo huku akizingatia kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa maji tiririka, kupaka vitakasa mikono na kutosalimiana na kukumbatiana.

Hayo yakifuatwa bila kuwapo kwa hofu, huku mbinu mbalimbali za kujiweka salama zikizingatiwa, ukiwamo suala la kumuomba Mungu, taifa linaweza kuendelea kuwa salama.

Karibu watu wote wanatambua kuwa virusi vya corona vipo, lakini visiwajaze hofu hadi kushindwa kufanya shughuli zao za kila siku, bali wazingatie tahadhari zinazotolewa na wataalamu wa afya.

## HABARI KITAIFA

# Vyama vyafunguka kauli ya IGP

**Na Enock Charles**

VYAMA vya Siasa nchini vimetoa ya moyoni baada ya kauli ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, kuwa atahakikisha uchaguzi mkuu wa mwaka huu unafanyika kwa hali ya amani na utulivu na kuwataka askari kutoruhusu mtu yeyote kucheza na bunduki kuwatisha Watanzania.

Akizungumza na gazeti hili, Mkuu wa Idara ya Habari na uenezi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tumaini Makene, amelitaka jeshi hilo kutozuia mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa ili kuweka mazingira sawa ya ushindani wa kisiasa.

"Iwapo IGP anataka kauli zake ziaminiwe na wadau wa uchaguzi vikiwamo vyama vya siasa na wananchi, Jeshi la polisi nchini liache mara moja kuvuruga shughuli za vyama vya siasa kama mikutano ya hadhara na kuacha kuingilia vikao vya ndani," alisema Makene.

Makene alimtaka Mkuu huyo wa Jeshi la Polisi kusimamia haki na katika uchaguzi huo kwa mujibu wa Katiba na Sheria bila kupendelea upande wowote ili kuhakikisha kunakuwapo na amani na utulivu wakati wote wa uchaguzi.

Naye, Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, amewataka polisi kuzingatia sheria na taratibu mbalimbali za jeshi hilo ikiwamo kutokutumia nguvu kabisa kwa wananchi au kutumia nguvu ya wastani pale tu inapolazimu kufanya hivyo.

"Sio tu suala la bunduki polisi hawapaswi kabisa kutumia nguvu kwa hiyo IGP anatakiwa aseme kwamba polisi waache kutumia mabavu au nguvu ya wastani pale inapobidi," alisema Ado

Naye, Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), Magdalena Sakaya, alipongeza hatua hiyo na kusema kuwa Jeshi hilo linapaswa kuhakikisha kwamba polisi hawaonekani kabisa katika eneo la kupigia kura ili wananchi wawe na amani katika zoezi hilo.

"Kama watakuwa serious (uhakika) na jambo hilo basi itakuwa vizuri kwa sababu katika baadhi ya nchi polisi katika vituo vya kupigia kura huwa hawaonekani kabisa," alisema Sakaya.

IGP Sirro aliwataka askari kutoruhusu mtu yeyote kucheza na bunduki kuwatisha Watanzania na wasiwe kero kwa wananchi wanaotii sheria na badala yake wawe mwiba kwa wasiotaka kufuata sheria.

Uchaguzi Mkuu unatarajia kufanyika Jumamosi ya mwisho ya Oktoba mwaka huu, na tayari maandalizi yameanza kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuandaa maadili ya uchaguzi yaliyopitishwa na wadau na kuchapishwa katika gazeti la serikali.




Mkurugezi wa Mauzo wa TBL Plc Kanda ya Kaskazini, James Bokella (kulia), akikabidhi sehemu ya msaada wa tani 10 za unga wa mahindi zilizotolewa na kampuni hiyo, kwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, mjini Moshi jana, kwa ajili ya kusaidia waathirika wa mafuriko yaliyotokea mkoani humo hivi karibuni. Kushoto ni Katibu Tawala wa mkoa huo, Dk. Khatibu Kazungu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ahukumiwa mwaka mmoja jela kuchapisha maudhui bila leseni

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imemhukumu mfanyabiashara Obadia Kwitega, kulipa faini ya Sh. milioni tano au kwenda jela mwaka mmoja baada ya kukiri kosa la kuchapisha maudhui mtandaoni bila kuwa na leseni ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Kadhalika, mahakama hiyo imemwamuru kulipa fidia ya Sh. milioni mbili.

Hukumu hiyo ilisomwa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Janeth Mtega.

Wakili wa Serikali Faraja Ngukah, alidai kuwa mshtakiwa aliandika barua kwa Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) na kufanya makubaliano ya kukiri kosa.

Hakimu alisema mahakama yake inamtia hatiani kwa kosa hilo.

Katika kesi ya msingi, kwitega, anadaiwa kuchapisha maudhui mtandaoni bila kuwa na leseni kati ya Januari 29, 2017 na Machi 29, 2019 mahali tofauti jijini Dar es Salaam kupitia televisheni ya Bongo Time's.

Ilidaiwa kuwa mshtakwia alichapisha maudhui hayo bila kuwa na leseni ya TCRA.

Kabla ya hukumu hiyo mshtakiwa alidai mahakamani ana familia na ndugu zake inamtegemea na kuomba apunguziwe adhabu.

# Takukuru yarudishia wananchi 13 mali zilizowekwa dhamana

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru), imerejesha mashamba na nyumba kwa wananchi 13 kutoka kwa mkazi wa Kijiji cha Makole, Nelson Ndalu, maarufu kwa jina la Osama (67), alizojipatia kwa kutoa mikopo kandamizi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Taasisi hiyo mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, jumla ya ekari 30 na nyumba mbili zimerejeshwa kwa wananchi kutoka kwa mtuhumiwa huyo ambaye anafanya biashara ya kukopesha fedha bila kufuata taratibu za ukopeshaji.

"Amekuwa akitoa mikopo kandamizi kwa wananchi wa Kata ya Chamkoroma, wengi walishindwa kurejesha mikopo hiyo yenye riba ya kuanzia asilimia 100 katika utaratibu maarufu kama 'Shilingi kwa Shilingi' na hivyo wakapoteza mashamba na nyumba zao walizoweka kama dhamana,"alisema.

Kibwengo alifafanua kuwa Takukuru Wilaya ya Kongwa baada ya kupata malalamiko hayo kutoka kwa mmoja wa wananchi mwezi Mei, mwaka huu ilifanya uchunguzi na kubaini kwamba Osama amekuwa na tabia hiyo kwa muda mrefu.

"Baadaye wakatokea wananchi wengine ambao nao walikuwa na malalamiko ya kudhulumiwa na hivyo kuifanya Takukuru kumshikilia mkopeshaji huyo ambaye Mei 27, mwaka huu, aliridhia kurejesha mashamba na nyumba mbili kwa wananchi hao 13 baada ya kulipwa fedha alizowakopesha," alisema.

Katika hatua nyingine, alisema taasisi hiyo imerejesha kiwanja namba 3, kitalu 'Q' Iyumbu New Town Centre kwa Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma baada ya uchunguzi kubaini kwamba aliyekuwa Mhasibu wa iliyokuwa mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) alimwezesha rafiki yake kupata kiwanja kwa njia ya udanganyifu.

"Uchunguzi wetu umeonyesha kwamba malipo ya awamu tatu yenye jumla ya Sh. milioni 43.6 yaliyoonekana kufanywa kulipia kiwanja hicho kati ya Juni, 2016 na Januari, 2017 na kukatiwa stakabadhi za malipo batili kutokana na fedha hizo kutopokelewa na risiti za mfumo wa Epicor ni za kugushi," alisema.

Vile vile, alisema rafiki huyo aliyeonekana kupewa kiwanja amekana kufanya malipo na kukirejesha kiwanja Halmashauri ya Jiji hilo na kuokoa kiasi hicho cha fedha.

# Corona yasimamisha uchimbaji dhahabu

**Sara Magesa, GEITA**

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu katika Kata ya Butobela wilayani Geita, wamesitisha shughuli za uchimbaji, kutokana na kukosa baruti za kulipua miamba.

Hali hiyo imesababishwa na janga la corona kwa kuwa malighafi hiyo inategemewa kutoka nje ya nchi.

Wameiomba serikali kuja na mpango mkakati wa kuanzisha kiwanda cha baruti katika Kanda ya Ziwa ili kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata bidhaa hiyo ambayo ni muhimu katika shughuli za ulipuaji wa miamba.

Wakizungumza wakati wakipokea msaada wa vifaa vya kujikinga na virusi vya corona uliotolewa na taasisi isiyo ya kiserikali ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo (FADev), walisema mbali na kukosa baruti pia wamekosa golori zinazotumika kwenye mtambo wa kusaga udongo wenye dhahabu.

Mkurugenzi wa Mgodi wa Mtalingi kijiji cha Nyakagwe, Kata ya Butobeka wilayani Geita, Hamza Mohamed, alisema ugonjwa wa corona umeathiri shughuli za wachimbaji wadogo kiuchumi, na kwamba katika mgodi wake amelazimika kupunguza wafanyakazi 100 baada ya kushindwa kuzalisha kutokana na changamoto ya upatikanaji vifaa.

Abdallah Mtalingi, alisema kukosekana kwa baruti za kulipua miamba kumekwamisha shughuli zao na kuiomba serikali kujenga kiwanda cha bidhaa zinazotumika kwenye shughuli za uchimbaji hususan wa dhahabu.

"Baruti zilikuwa zinaagizwa kutoka nchi za Afrika Kusini na India na hapa nchini ni kampuni moja tuu ilikuwa inaagiza, lakini uwapo wa corona wafanyabiashara wakubwa walinunua kwa wingi na kutunza... sasa sisi wadogo tumekosa pa kununua, hatuwezi kufanya kazi zetu," alisema Mtalingi.

Alisema mbali na kukosa baruti, pia biashara yao imedorora baada ya wafanyabiashara wakubwa kusitisha kutoa fedha za kuwekeza kwenye uchimbaji.

"Ili sisi tuchimbe lazima tupate fedha kutoka kwa wafanyabiashara wakubwa ambao wanatupa vifaa na sisi tukifanya kazi tunawauzia mali kwa hiyo wao wanapata na sisi tunapata, lakini hii corona wameogopa kuwekeza fedha zao kwenye dhahabu, hii inatukwamisha sana," alibainisha.

Mkurugenzi wa FADev, Tinna Mwasha, alisema taasisi yake imeamua kutoa vifaa kwa wachimbaji wadogo ili kuwanusuru na maambukizo ya corona kutokana na kundi hilo kuwa na mwingiliano mkubwa wa watu.

Vifaa vilivyotolewa ni barakoa, vitakasa mikono, ndoo za maji na sabuni na machapisho ya namna ya kujikinga na virusi hivyo.



Mkurugenzi wa Shirika linalotetea Haki za Wanawake na Watoto la Agape Mkoa wa Shinyanga, John Myola (kushoto), akitoa elimu namna ya kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka kwa Mohamed Ally, ambaye ni miongoni mwa watu wenye ulemavu waliopewa elimu hiyo, ili kujikinga na maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona, mkoani humo jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Kanisa latoa chakula cha mil. 19/- kusaidia watoto mazingira magumu

**Na Welingtone Masele, TABORA**

KANISA la Tanzania Assemblies of God (TAG-Kitete), kwa kushirikiana na Shirika la Compassion linalohudumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu, limetoa msaada wa chakula chenye thamani ya Sh. milioni 19.3.

Akikabidhi msaada huo kwa familia 217 za watoto hao, Mchungaji Kiongozi wa kanisa hilo, Paul Meivukie, alisema chakula hicho kimetolewa kama ishara ya upendo kwa watoto wote wanaoishi katika mazingira magumu wanaolelewa kituoni hapo.

Alisema chakula kilichotolewa ni kilo 11,718 za mahindi na kilo 4,340 za maharagwe, vyote vikiwa na thamani ya Sh. 19,313,000.

Kupitia msaada huo kila familia imepewa madebe matatu ya mahindi na debe moja la maharagwe ili kuwasaidia katika kipindi hiki cha ugonjwa wa homa ya mapafu (Covid-19).

Meivukie alimpongeza Rais Dk. John Magufuli kwa msimamo wake thabiti wa kiimani na kutokubali kuyumbishwa na mtu yeyote katika kipindi hiki kigumu cha mapambano ya ugonjwa huo.

Alisisitiza kuwa msimamo huo na juhudi kubwa alizozifanya ikiwamo kutangaza maombi ya siku tatu kwa waumini wa madhehebu yote ya dini nchini, kuliombea taifa ili Mungu aliepushe taifa na ugonjwa huo.

Aliwataka wazazi na walezi wa watoto hao kuwaelimisha juu ya ugonjwa huo kipindi hiki ambacho wamepumzika nyumbani, pia kuhimiza watoto wao kumtegemea Mungu ili awalinde na mabaya yote.

Mwenyekiti wa Kamati ya Wazazi wa Watoto hao, Mrema Warioba, alilishukuru kanisa na Shirika la Compassion kwa msaada huo, alibainisha kuwa chakula hicho kitawasaidia sana hasa katika kipindi hiki ambacho watoto wako nyumbani.

# Wakulima walia kushindwa kusafirisha mazao

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

WAKULIMA wa mazao mbalimbali wilayani Mvomero, wamesema licha ya kutumia nguvu kubwa ya kuzalisha mazao, wanakabiliwa na changamoto ya ubovu wa barabara ya kusafirisha mazao yao kutoka shambani.

Mmoja wa wakulima hayo, Mwanaidi Hamza, alisema kuwa licha ya kutumia nguvu kubwa kuwekeza kwenye kilimo cha mpunga, changamoto ya ubovu wa barabara inawafanya washindwe kusafirisha mpunga kupeleka kwenye maghala.

"Ubovu wa barabara unasababisha wakulima wengi wa mazao hususani mpunga kushindwa kusafirisha zao hili kwenda kwenye maghala ya kuhifadhia yaliyojengwa na serikali," alisema Mwanaidi.

Alisema kutokana na ubovu huo hali hiyo inaweza kuleta hasara kwao kwasababu ya kushindwa kufikisha mazao yao ghalani kwa wakati na kuiomba serikali kuingilia kati ili waweze kuokoa mazao yao.

Alisema wakulima wa kijiji cha Bungoma kata ya Mkindo wameishukuru serikali kwa kuwajengea ghala lenye uwezo wa kuhifadhi magunia 40,000 kwa wakati mmoja, lakini changamoto iliyopo ni ubovu wa barabara.

Naye Khamis Funge alisema wakulima wa kijiji hicho wapo kwenye wakati mgumu na hawajui hatima yao kwa kuwa mazao yao yapo kwenye hatari ya kuharibika shambani.

Funge alisema wakulima wa kijiji hicho hutegemea kilimo kama njia ya kujipatia kipato, hivyo kitendo cha kukosa barabara kinawafanya wakose uhakika wa kupata kipato.

Alisema kuwa kutokana na changamoto hiyo baadhi ya wakulima wanavuna mpunga shambani pamoja na mazao mengine na kuyasomba kwa baiskeli, pikipiki na punda.

Kwa upande wake Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura), Mhandisi William Lameck, alisema kero hiyo imefika ofisini kwake na ameijumuisha kwenye bajeti ijayo.

Aliwataka wakulima hao kuendelea kuzalisha mpunga na mazao mengine kwa wingi na kwa maslahi ya taifa kwa kuwa changamoto ya ubovu wa barabara inashughulikiwa.

HABARI KITAIFA

## DC Kawawa aonya watendaji vitambulisho

**Na Julieth Mkireri, CHALINZE**

MKUU wa Wilaya ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani, Zainabu Kawawa, amewaonya watendaji wataokwamisha usambazaji wa vitambulisho kwa ajili ya wajasiriamali.

Kawawa alitoa onyo hilo mjini Lugoba wakati wa makabidhiano ya vitambulisho na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chalinze, Zainabu Makwinya, ambapo alisema hatokuwa na msamaha kwa yeyote atakayebainika kuwa kikwazo katika ugawaji wa vitambulisho hivyo.

Alisema vitambulisho hivyo vilivyotolewa na Rais John Magufuli kwa wajasiriamali wadogo, vinalenga kuwaondolea changamoto walizokuwa wakipambana nazo kutoka kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Alisema, katika wilaya yake wamepokea vitambulisho 10,106, ambavyo vinagawiwa katika Halmashauri za Bagamoyo na Chalinze.

## Utafiti waanika ujazo wa maji Ziwa Nyasa

**Na Innocent Ng'oko, MBEYA**

LICHA ya usawa wa maji kuendelea kupanda katika Ziwa Nyasa kati ya Januari na Aprili mwaka huu, takwimu za ujazo wa maji zinaonyesha kuwa hali hiyo haijaweza kufikia wastani wa muda mrefu wa kiwango cha maji kujaa katika ziwa hilo.

Ofisa Maji Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Nyasa, Mhandisi Alice Engelbert, alisema utafiti wa kitaalamu juu ya kuongezeka kiwango cha maji katika Ziwa Nyasa inaonyesha kuwa hadi kufikia Aprili, 2020 kiwango cha ujazo wa maji kilikuwa mita 477.68.

Alice alisema Januari mwaka huu hali ya ujazo wa ziwa hilo ilikuwa mita 476.45, Februari ziwa hilo lilijaa na kufikia ujazo wa mita 476.78 na Machi mwaka huu ziwa hilo lilijaa na kufikia ujazo wa mita 477.25.

"Pamoja na usawa wa maji kuendelea kupanda katika Ziwa Nyasa kwa Januari hadi Aprili mwaka huu, hali hiyo haijaweza kufikia wastani wa muda mrefu wa kiwango cha maji kujaa katika Ziwa Nyasa," alisema Mhandisi Alice.

**Ofisa Maji Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Nyasa, Mhandisi Alice Engelbert, alisema utafiti wa kitaalamu juu ya kuongezeka kiwango cha maji katika Ziwa Nyasa inaonyesha kuwa hadi kufikia Aprili, 2020 kiwango cha ujazo wa maji kilikuwa mita 477.68.**

# Serikali yaagiza kuwekwa uzio minada ya mifugo

**Na Welingtone Masele, KALIUA**

SERIKALI wilayani Kaliua, mkoani Tabora imeagiza kuwekwa uzio kwenye minada yote ili mifugo yote inayopelekwa ilipiwe ushuru.

Agizo hilo limetolewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Abel Busalama, alipokuwa akiongea na watendaji pamoja na wataalamu wa halmashauri hiyo.

Alisema, halmashauri hiyo imekuwa kinara wa ukusanyaji mapato katika Mkoa wa Tabora kwa takribani miaka mitatu mfululizo kutokana na usimamizi madhubuti wa mapato hayo.

"Nina uhakika tukijenga uzio katika minada yetu yote tutadhibiti mianya ya wizi na kuongeza makusanyo kutoka mapato ya sasa ya Sh. milioni 500 hadi kufikia Sh. bilioni moja," alisema.

Aliwataka watendaji wote kuhakikisha magari ya mizigo yanayopita katika mageti (vizuizi) barabarani yanakaguliwa na mapato yote yanayopatikana kutokana na faini au ushuru yanatunzwa vizuri.

Kwa kutambua kuwa minada ni chanzo kizuri sana cha mapato kwa halmashauri hiyo, Mkuu wa Wilaya alishauri uongozi wa halmashauri hiyo kuangalia uwezekano wa kuanzisha mradi mwingine wa mnada kwa kuwa hata waziri mwenye dhamana alishaahidi kuwasaidia kutumia mtandao wa kielektroniki kukusanya mapato.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. John Pima, alimhakikishia mkuu huyo kuwa watatekeleza maelekezo na ushauri aliowapa kwa manufaa ya wana Kaliua wote.

Alionya kuwa mtendaji yeyote atakayekiuka maadili ya utumishi wa umma na kujiingiza katika mambo yasiyofaa ikiwamo kutumia mapato aliyokusanya kinyume na utaratibu, atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwamo kufikishwa katika vyombo vya sheria.



Menyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Emmanuel Charahani (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, mjini Kahama jana, wakati akitoa ufafanuzi wa namna ya kuwaingiza wakulima wa mpunga na mahindi kwenye Amcos au mfumo wa stakabadhi ghalani. **PICHA SHABAN NJIA**

# Ukarabati barabara nne kuanza Ubungo

**Na Beatrice Moses**

JUMLA ya Sh. milioni 145 zinatarajiwa kutumika katika utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa barabara nne zenye maeneo korofi yaliyowahi kuzusha ugomvi kati ya abiria na madereva wa bajaji.

Barabara hizo zilizoharibiwa na mvua zipo Kata ya Saranga, wilayani Ubungo zimeanza kukarabatiwa, hatua ambayo inatarajiwa kuwapunguzia kero na gharama wakazi wa maeneo hayo.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini (Tarura) Manispaa ya Ubungo, Laynas Sanya, jana alipita kukagua utekelezaji mradi huo, ambapo alitaja barabara zinazohusika ni Suka, Saranga, Bonyokwa na Takukuru Ruguruni.

Sanya alisema utekelezaji wa mradi huo unahusisha uchongaji wa barabara, uwekezaji wa vifusi na mifereji kwenye baadhi ya maeneo hasa yanayotajwa kuwa korofi.

"Mkandarasi amepewa maelekezo ya jinsi ya kutekeleza mradi huu, naamini atazingatia, mvua zilionyesha zimeathiri maeneo mengi ya barabara hizo ukarabati huu utasaidia kuboresha miundombinu na kusaidia maeneo hayo kupitika," alisema Sanya.

Alisema ukarabati wa barabara ya Saranga yenye urefu wa Km 3.5 inayohusisha Mtaa wa Ukombozi inagharimu Sh. milioni 25.7, pia barabara ya Suka ambayo inahusisha Mtaa wa Upendo na Saranga yenye urefu Km 2.2 imetengewa Sh. mlioni 18.

Wenyeviti wa mitaa mitatu iliyopo katika Kata ya Saranga wametoa maoni yao kuhusu mradi huo wakibainisha kuwa ili ufanikiwe, wanapaswa kushirikishwa kikamilifu ikiwamo kupewa mchanganuo wa utekelezaji unavyobanwa kuwa.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wenyeviti hao Mtaa wa Upendo, Saranga na Ukombozi, wamebainisha kuwa hawajaona mchanganuo wa ukarabati huo unapaswa kupunguza kero ambazo zimekuwa zikiwakabili wakazi wa maeneo yao hasa wakati wa mvua.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Upendo, Gwelino Kalinga, alisema alipata taarifa kuwa ukarabati huo utahusisha umwagaji wa kifusi, lakini bado hajaona kilichomwagwa.

"Natamani kuona mradi huu unafanikisha kuondoa ama kupunguza kero kwa wananchi wangu kulingana na bajeti iliyotejwa, kwani mradi uliopita kuna mahali panaitwa daraja la mbao kulijengwa daraja kwa shilingi milioni 35 tayari kwa mvua hizi limeanza kuharibika hivyo linaweza kusababisha usumbufu kwa wananchi tena," alisema Kalinga.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Saranga, Godwin Muro, alijaribu kufuatilia ili kujua ukarabati huo utakavyokuwa hasa akizingatia kuwa katika mtaa wake kuna maeneo korofi ambayo yamewahi kusababisha vurugu.

Alisema vurugu zilizuka baada ya madereva wa bajaji kupandisha nauli kutoka Sh. 500 hadi 1,000 ambayo wananchi waligomea.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Ukombozi, James Mulokozi, alisema emeona diwani ndiye anashirikishwa kwa karibu, wakati yeye alijulishwa kwa njia ya simu tu kuwapo kwa mradi huo badala ya kupewa mchanganuo wa utekelezaji utakavyokuwa katika eneo lake.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Lameck Kisare, ameahidi kufuatilia kwa karibu hatua za ukarabati huo, ili kuhakikisha matumizi mazuri ya fedha za serikali.

HABARI KITAIFA

KWA UFUPI

## Utalii kuongeza mapato Kisarawe

Na Futuna Seleman, KISARAWE

SERIKALI wilayani Kisarawe mkoani Pwani imeweka mkakati wa kuongeza mapato yake kupitia sekta ya utalii, kwa kuweka vivutio vya kutosha ikivishirikisha vikundi vya utamaduni.

Imesema vikundi hivyo vitatoa burudani katika maeneo watakayokuwapo watalii ikiwamo yenye mvuto wa utalii wilayani humo.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Jokate Mwegelo, aliyasema hayo alipofanya ziara ya ukaguzi kwenye maeneo yenye mandhari ya vivutio vya utalii katika kijiji cha Boga Vikumburu wilayani humo.

Kwenye ziara hiyo, Jokate aliongozana na Kiongozi wa Chama cha Waongoza Watalii Kusini mwa Tanzania, George Mbwambo, ili kukagua barabara itakayotumiwa na watalii kuelekea Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere.

Alisema ili kuvutia utalii wilayani humo ni muhimu ujenzi wa barabara ya Kisarawe- Mloka hadi katika Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere iliyomegwa kutoka Hifadhi ya Taifa ya Pori la Akiba la Selous ijengwe kwa kiwango cha lami.

## DAS aipongeza Ilala hati safi

Na Beatrice Shayo

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, ameipongeza Manispaa ya Ilala kwa kupata hati safi ya mahesabu kwa miaka minne mfululizo na kuwataka watendaji kuongeza ufanisi ili kupata matokeo bora zaidi.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo, Kunenge alisema Ofisi ya Mkoa imeridhika na utendaji wa kazi wa manispaa kupitia miongozo mbalimbali iliyotolewa na Baraza la Madiwani.

Alisema muda umefika kwa watendaji wa manispaa hiyo kubuni mipango zaidi itakayoisaidia kuongeza mapato.

"Kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa napenda kuwapongeza kwa dhati kutokana na juhudi mbalimbali mnazozichukua kuhakikisha manispaa hii inaendelea kupata hati safi za mahesabu, hatua hii isiwafanye mbweteke kuendelea kutekeleza majukumu yenu ipasavyo," alisema Kunenge.

Aidha, aliwapongeza watendaji pamoja na madiwani kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo iliyoainishwa katika ilani ya CCM, ikiwamo ujenzi wa soko la kisasa la Kisutu, machinjio ya Vingunguti na miradi mingine.

# Bodi ya Kahawa kutafuta wanunuzi binafsi

Na Mwandishi Wetu, MARA

BODI ya Kahawa imetakiwa kutafuta wanunuzi binafsi kadri iwezavyo ili kuongeza ushindani lengo ni wakulima wauze kahawa kwa bei nzuri isiyokandamizi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, alipokuwa akizungumza kwenye kikao kazi na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa, Prof. Jamali Adam.

Alisema wanunuzi binafsi wataruhusiwa kununua kahawa kupitia vyama vya ushirika badala ya kwenda moja kwa moja kwa wakulima.

Alibainisha hatua hiyo itasaidia kukabiliana na unyonyaji dhidi ya wakulima wa kahawa pamoja na mazao mengine mkoani Mara.

"Mkulima yeyote akisikia bei nzuri ya kahawa lazima atauza...hawezi kwenda kwenye bei ndogo wakati ameona kuna mahala kuna bei nzuri inayoendana na jasho lake," alisema.

Alisema serikali iliamua kuanzisha ushirika kwa ajili ya wakulima kuuza mazao yao kwa bei nzuri, hivyo wanunuzi binafsi ni ruksa, lakini wanapaswa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

"Uuzaji wa Mazao ya wakulima kupitia vyama vya ushirika tumeuweka ili kama wakulima wakiibiwa au kupunjwa...sisi iwe rahisi kumpata muhusika na tunachukua hatua kali dhidi ya wote watakaofanya ubadhirifu, lakini tukimkuta mnunuzi binafsi ameingia mpaka shambani ni kama ameingia chumbani atapata balaa," alisisitiza Malima.

Sambamba na hilo, aliipongeza bodi hiyo kwa kutoa miche 40,000 kwa ajili ya mkoa wa Mara, huku akisisitiza umuhimu wa bodi hiyo kuwaongezea wakulima miche mingi zaidi ili kuongeza uzalishaji wa kahawa nchini.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi, Prof. Adam, alisema kuwa bodi imejiwekea malengo muhimu ya kuongeza uzalishaji wa kahawa nchini, na kuwa na bei nzuri.




Mratibu wa Afya Shuleni kutoka Idara ya Afya ya Halmashauri ya Mji wa Masasi, mkoani Mtwara, Theresia Moyo, akitoa elimu ya kujikinga na ugonjwa wa corona kwa wanafunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (FDC), Masasi jana. **PICHA: HAMISI NASIRI**

# GGML yatoa mil. 100/- za ujenzi wa chuo kikuu

Na Mwandishi Wetu

KATIKA kukuza sekta ya elimu ya juu nchini, Kampuni ya Geita Gold Mining Ltd. (GGML) kupitia sera yake ya uwajibikaji kwa jamii, imetoa Sh. milioni 100 kusaidia ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) Mkoa wa Geita.

Awamu ya kwanza ya mradi huo inajumuisha ujenzi wa jengo la utawala linalojumuisha chumba cha mikutano cha viongozi, maktaba, chumba cha maabara ya kompyuta na ofisi nyingine tano.

Pia kiasi hicho cha pesa kilichotolewa na GGML ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi na malipo ya mafundi ujenzi.

Makamu wa Rais Maendeleo Endelevu katika kampuni hiyo, Simon Shayo, alisema uwezeshaji huu unatarajiwa kufaidisha wanafunzi 500 wanaotokea katika vituo vitatu vya Mkoa wa Geita ambavyo ni Chato, Nyang'wale na Geita mjini.

Alisema GGML kwa kushirikiana na wananchi, imeamua kuunga mkono juhudi za serikali kufadhili mradi huo kwani mbali na kuongeza mazingira bora ya upatikanaji wa elimu, pia utazalisha wahitimu bora wenye weledi ndani ya jamii watakaokuwa na uwezo wa kusukuma gurudumu la maendeleo ya Taifa mbele kwa kupitia elimu waliyoipata.

Alisema Chuo hicho Tawi la Mkoa wa Geita, kama vilivyo vyuo vingine, kimekuwa kikifanya shughuli zake katika majengo ya kukodi, ambayo hutumika kama madarasa na ofisi za utawala.

"Kwa ufadhili huu, tuna hakika kwamba chuo kikuu kitapunguza gharama za uendeshaji na kuboresha ufanisi. Zaidi ya hayo itaunda uhusiano mzuri kati ya wanafunzi kutoka Geita na vyuo vingine 30 vya OUT. Mradi huu moja kwa moja unasaidia serikali kufikia lengo la 4 la maendeleo endelevu (SDGs), ambalo ni upatikanaji wa elimu bora ifikapo 2030 kama ilivyotarajiwa," alisema Shayo.

Mkurugenzi wa OUT Mkoa wa Geita, Ally Abdu, aliishukuru GGML kwa msaada huo, ambao unaongeza mazingira mazuri ya kusoma na kukidhi idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu ambao wanaongezeka kila mwaka.

ama
ALHAMISI JUNI 4, 2020
AFYA NA MAZINGIRA


Ukurasa 12

**Corona 'kupumua' ina ujumbe gani kwa safari kuu ya afya?**


Ukurasa 13

Kwa nini mtu anatoa harufu kinywani, koo lahifadhi jiwe?



Ukurasa 14

**Bosi Mkuu TFS: Tumenufaika na misitu, vikwazo vyetu hivi...**

AFYA

# Hatimaye, vita fistula imeanza kuwasha taa ushindi kimataifa

**Na Yasmine Protace**

• Nchi imevuka mstari wa mafanikio



Washiriki Siku ya Fistula Duniani, katika moja ya hospitali jijini Dar es Salaam, inayofanyika kila Mei 23 ya mwaka. **PICHA: MTANDAO.**

FISTULA imo katika orodha ya magonjwa hatari. Ni tatizo kitaifa na kimataifa ambayo vita yake inapangwa kwa nguvu kubwa, kupitia ngazi hizo hizo zilizotajwa.

Vita hivyo, imeratibiwa siku yake ya kuadhimisha kimataifa; Mei 23 kila mwaka, ikipatiwa kaulimbiu maalum kwa mwaka husika.

Katika maadhimisho ya mwaka huu yaliyofanyika wiki mbili zilizopita, inaangukia kauli: "Tokomeza unyanyasaji wa kijinsia;Tokomeza Huduma ya Afya Isiyo na Usawa; Tokomeza Fistula sasa."

Fistula asili yake zaidi inawaangukia baadhi ya wanawake wajawazito na hasa kwa wanaoshindwa kuhudhuria kliniki kwa wakati.

Kanuni ya afya inaongoza kwamba mwanamke anayejihisi ujauzito, anatakiwa kufika hospitali kuanza kliniki kwa wakati, ikiwa njia mojawapo ya kufanikisha mchakato wa uzazi kwa namna sahihi. Katika kupambana na ugonjwa huo, serikali kupitia nyenzo zake na wadau wa afya, imekuwa ikitoa elimu jinsi ya kupambana na ugonjwa huo.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anaeleza habari njema kuwa wajawazito wameipokea elimu na sasa serikali imepiga hatua dhidi ya ugonjwa huo.

Pia, inaelezwa baadhi ya wanawake wamekuwa wakipatwa na fistula kwa sababu ya kukabiliwa na matukio ya ukatili wa kingono.

Rai iliyoko kiafya ni kwamba, fistula inatibika na kinamama katika ujauzito wao wanatakiwa kuhudhuria kliniki wafanyiwe uchunguzi unaofanikisha afya ya mama na mtoto.

> **Katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015 hadi Desemba, 2019 wanawake zaidi ya 5,500 wametibiwa fistula.**

Waziri Ummy katika kauli yake Siku ya Fistula mwaka uliopo, anawahimiza kinamama wenzake kubadilika kwa kuacha tabia ya kujifungua majumbani, wakizingatia mbadala wa hospitalini.

Anataja takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) za mwaka 2018, kuna wanawake takribani milioni mbili wanaoishi na fistula duniani kote.

Pia, inakadiriwa kwamba licha ya kuwapo wagonjwa wapya kati ya 50,000 na 100,000 kila mwaka, juhudi za kutibu fistula zinagota kwa wagonjwa 20,000 peke yake.

Kuhusu takwimu za nchini, waziri anasema kuna makadirio ya kuwapo wagonjwa 2,500 kitaifa wanaopata fistula kila mwaka na kati yao wanaopatiwa matibabu ni takribani kinamama 1,000 tu (asilimia 40).

Licha ya kutofikia nusu ya wagonjwa husika, mtazamo wa wastani nao unaijulisha Tanzania imeshapiga hatua kubwa kulinganisha na wastani uliopo duniani.

"Katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015 hadi Desemba, 2019 wanawake zaidi ya 5,500 wametibiwa fistula

"Mafanikio haya yanatokana na kampeni iliyoendeshwa kwa ushirikiano baina ya serikali na wadau ambayo imeweka mabalozi wa fistula zaidi ya 3,000 nchi nzima wanaosaidia kuratibu rufani na usafiri kwa wagonjwa kwenda hospitali zinazotoa huduma ya fistula," anasema Ummy.

Aidha, Waziri Ummy anataja idadi ya Wanawake wanaojitokeza kutibiwa fistula kwenye hospitaii zinazotoa huduma zimepungua kwa theluthi moja, kati ya mwaka 2015 hadi mwaka jana.

Anasema huduma za fistula nchini zinapatikana kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) na CCBRT, jijini Dar es Salaam; Bugando (Mwanza); Hospitali ya Kanda ya Rufani - Mbeya; Hospitali ya Nkinga (Tabora); KCMC (Moshi); na Kivulini Maternity Center iliyoko Arusha.

"Tuna wataalamu waliobobea kwenye tiba ya fistula kwenye hospitali hizi. Hatua hii imetokana na kuimarika huduma za afya ya mama wajawazito, ikiwa ni pamoja na upatikanaji huduma za upasuaji wa dharura," anasema Waziri Ummy.


"Mama mjamzito endapo atawahi kliniki mapema kwa ajili ya uchunguzi wa maendeleo ya afya yake na mtoto na kuhakikisha anajifungulia katika kituo cha kutoa huduma za afya, atapunguza uwezekano wa kupata tatizo la fistula," anasema.

Waziri haonyeshi uvivu kwa kinamama wenzake, akitawaka kukimbilia kliniki mapema kukamilisha maudhurio yote yanayopaswa ikiwamo kujifungua katika vituo vya afya.

Anasema, kutokomeza fistula nchini kunahitajika juhudi za pamoja za wadau mbalimbali, wakiwamo watumishi wa afya wa ngazi zote, wizara mbalimbali, wadau wa maendeleo, wanahabari na asasi zinazojihusisha na matibabu yake.

AFYA

# Corona 'kupumua' ina ujumbe gani kwa safari kuu ya afya?



Ilivyo hali halisi ya kuikabili corona duniani. **PICHA: MTANDAO**

**Na Beatrice Philemon**

***WIKI hii kidato cha sita na vyuo, zimefunguliwa. Pia, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ametangaza kuwapo wagonjwa wasiozidi wanne kitaifa, wote jijini Dar es Salaam, vituo vingi vya karantini vimebaki vitupu. Hiyo ina maana gani kitaifa na kimataifa? Makala kutoka shirika la BBC, ina uchambuzi wenye uwanda wa tafsiri hiyo kimataifa.***

"Mlipuko wa pili wa maambukizo ya virusi vya corona, sio tena suala, ikiwa linaweza kutokea badala yake ni lini litatokea na athari yake itakuwaje," anasema Dk. Jennifer Rohn, anayefuatilia janga hilo

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema huenda maambukizo mapya yakaendelea kwa kipindi kirefu na udhibiti wake unahitaji juhudi za pamoja kimataifa.

Hivi karibuni Umoja wa Ulaya (EU) inayopambana na ugonjwa wa Covid-19, ilipendekeza kwamba Ulaya inastahili kujiandaa kwa mlipuko wa pili. Swali lililopo ni lini itatokea na athari zake zitakuwa na ukubwa gani?

Kwa mujibu wa gazeti la The Guardian la Uingereza, serikali zote duniani zinapaswa kujiandaa kwa uwezekano wa wimbi la pili la virusi vya corona, huku macho yakiangazia zaidi Asia Mashariki.

### DARASA LIPI?

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Tedros Adhanom, anasisitiza kujifunza kuhusu Asia Mashariki, ikilinganishwa na kwingineko duniani.

> **Sio kwamba tunahitaji tu kujua wale waliopata maambukizo ambayo unaweza kufahamu kupitia vipimo vya kwenye mdomo, pia unahitaji kupima kupitia kinga ya mwili, ili kufahamu ni nani aliyetangamana naye.**

Wataalamu wa WHO wanaofuatilia eneo hilo, wanasema kuna umuhimu mkubwa wa kuwapata, kuwatenga, kuwapima na kuwafuatilia waathirika na hata kuwaweka karantini.

Dk. Rohn, mtaalamu wa virusi na magonjwa ya kuambukiza kutoka Chuo Kikuu cha London, anakubaliana na hilo akifafanua:

"Data kutoka Asia tumeona namna pekee ya kudhibiti wimbi la pili la maambukizo, ni kupitia upimaji wa kasi kwa raia, kuwatafuta na kisha kuwaweka karantini."

Anatumia mfano wakati Korea Kusini ilikuwa kitovu cha corona, lakini serikali ilichukua hatua kuwapima watu kupitia mfumo wa simu na upokeaji habari kutoka satelaiti, wakawatafuta walioathirika.

Inaelezwa ufanisi wake ulithibitika, pale maambukizo mapya yaliporekodiwa mwezi uliopita, pakihusisha vilabu maarufu vya usiku na wamewafuatilia watu zaidi ya 11,000.

Darasa la pili ni umuhimu wa uchukuaji taarifa, zikatafsiriwa na kisha kutafitiwa kutoka maeneo penye uwepo wa virusi zaidi kama nchi za China, Japan na Korea Kusini.

Profesa Alistair McGuire, kutoka Shule ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha London, anasema corona ina tabia ya kubadilika, ikilinganishwa na magonjwa mengine ya virusi kama vile Sars na Ebola.

Tatu, kuna suala la kufahamu kirusi kipya kitakavyobadilika baada ya kulegezwa masharti na Profesa McGuire, anaiangaza bara Asia kwa angalizo: "Tusiwe na matumaini sana."

Eneo la Hokkaido nchini Japan, lilikuwa la kwanza kutekeleza karantini Februari iliyopita na mwezi mmoja baadaye, maambukizo mapya yalishapungua maradufu na Aprili shule zilifunguliwa, lakini, mwezi mmoja kupita, hatari iliibuka na kuwekwa tena katika karantini.

Kupitia mtazamo huo, Dk. Rohn, anatoa ufafanuzi: "Hata kwa nchi zinazoonekana mlipuko huo umedhibitiwa kwa sababu masharti yamelegezwa maambukizo, yanaanza kuongezeka. Hili ni jambo litaalotokea kote duniani".

"Kuna ujumbe unaotolewa na wataalamu wa afya kila wakati, kwamba tumejifunza kutoka Asia, kupima ni hatua ya msingi," anahimiza Dk. Rohn na anaendelea:

"Korea Kusini ilipata ufanisi mkubwa katika kudhibiti virusi kwa sababu ya hatua ya upimaji wa watu wengi, kuwatafuta na kuwaweka karantini."

Nchi hiyo ilianza mfumo wa upimaji bure na kufikia kiwango kupima wastani wa watu 10,000, ambayo ilikuwa na mfanikio makubnw

Profesa Ooi Eng Eong, mtaalamu wa magonjwa ya kuambukiza katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Singapore, ana unaungana na hija hiyo, akisema ni jambo la kuigwa.

Nchi za Magharibi zilizofuata mfumo wa upimaji wa Asia Mashariki, mathalan Ujerumani, kitaalamu zinaelezwa zimeufanikiwa kupunguza vifo, ikilinganishwa na wenzao kama Uingereza na Hispania.

"Sio kwamba tunahitaji tu kujua wale waliopata maambukizo ambayo unaweza kufahamu kupitia vipimo vya kwenye mdomo, pia unahitaji kupima kupitia kinga ya mwili, ili kufahamu ni nani aliyetangamana naye," anafafanuaProfesa McGuire.

### MIFUMO KUJIHAMI

Taiwan na Japan, vipimo vyao vilionyesha walioambukizwa na waliopata nafuu walifuatiliwa, wakatafutwa na kuwekwa karantini, hivyo takwimu zikaonyesha nani aliyeambukizwa, aliko na maambukizo yanavyosambaa haraka.

Singapore ilionyesha makubwa kwa kuwatafuta na kuwasiliana na maelfu kwa kutumia picha za video kwenye CCTV na njia nyinginezo wakijitenga hadi pale majibu yatakapotoka.

Waliojitenga walipigiwa simu mara kadhaa kwa siku na wakati mwingine walihitajiwa kutuma picha za kuthibitisha mahali waliko.

Nchini Hong Kong, kulishuhudiwa wakitumia mfumo usio wa kawaida, bangili za kielektroniki kwa wanaoingia nchini kutoka mataifa mengine.

"Unachohitaji kuangalia ni kile kilichotokea Korea Kusini, nchi yenye sera bora. Baada ya kulegeza masharti, mtu mmoja alifanikiwa kuambukiza watu zaidi ya 100 kwa wikendi moja tu."

Hivi sasa nchi hiyo inajiandaa na uwezekano wa kutokea mlipuko mwingine, baada ya maambukizo mapya ya Mei 19 katika hospitali kubwa jijini Seoul na ilishabaini maambukizo tisa, mara ya pili.

### AFYA YA UMMA

Mtaaluma Profesa Judit Vall, anayefuatilia mifumo ya kukabili corona, katika Chuo Kikuu cha Barcelona, Italia ana maoni kwamba sekta ya afya imethibitisha inaweza kufanya mabadiliko ya haraka.

Anasema China ilijenga hospitali yenye vitanda 1,000 mjini Wuhan, kitovu cha ugonjwa corona, kazi iliyofanyika kwa siku nane.

"Hospitali na vituo vya kutoa huduma zingine za msingi duniani wamejifunza anasema Profesa Vall

"Maambukizo huja wakati wa kuondoa vizuizi. Hiki ndicho kinachofanyika unapokuwa na virusi vipya na hakuna kinga miongoni mwa watu," anasema Dk. Rohn.

"Si tu tunachoweza kujifunza kutoka nchi nyingine, lakini tunaweza kujifunza nini kutokana na matukio yaliyopita," anatoa angalizo kitaalamu, Dk. Laia Maynou, kutoka nchini Hispainia.

Mtaalamu huyo, anasema kuna darasa la umma kujifunza kwenye mlipuko wa mafua nchini Hispania mwaka 1918, ukafananishwa na kilichoko sasa.'

### KUTOKA WHO

Kurugenzi ya WHO, inayosimamia udhibiti wa corona ukanda wa Magharibi mwa Pasifiki, inahimza hatua si vipimo pekee, bali kuna uepukaji umma kuchangamana, hatua iliyotbibitisha mafanikio

WHO inaeleza kuna njia nyingi za kujifunza kutoka mlipuko wa homa ya Sars mwaka 2003 na inasisitiza bado kuna hatari hadi itakapopatikana chanjo halisi kimataifa.

AFYA

# Kwanini mtu anatoa harufu kinywani, koo lahifadhi jiwe?

Na Jackson Paulo

TATIZO la kutokwa harufu mbaya kwenye kinywa limekuwa likiwasumbua watu wengi, japo sehemu kubwa wanashindwa kujua chanzo chake na hata tiba sahihi.

Kuna mambo yanayochangia hali hiyo, lakini chanzo kikubwa ni uwepo wa mawe kwenye tezi ya koo ambayo kitaalamu inajulikana 'tonsil stones'.

Inaelezwa kitaalamu, mawe hayo hayana hatari kubwa na mtu anaweza kuishi nayo kwa kipindi kirefu bila ya tiba. Hiyo ni sababu watu wengi wanaendelea kudumu na harufu mbaya kinywani kwa muda mrefu, pale wanapokosa matibabu.

Kuna wakati hali hiyo inampa muathirika harufu mbaya kinywani kiwango cha kushindwa kuficha kinachomkabili, maana harufu imetawala.



Daktari wa koo akimhudumia mgonjwa wake. **PICHA: MTANDAO**

### NINI CHANZO?

Tezi kwenye koo 'tonsils' ni sehemu ya mfumo wa ulinzi wa mwili, inayosaidia kuzuia vimelea vya kutoka nje vilivyoingia mwilini kwa njia ya mlo au kuvuta hewa.

Vitu kama vipande vidogo vya chakula, uchafu na chembe nyinginezo zinaweza kukwama na mtu akajikuta vinabaki katika mikunjo ya tezi za kooni.

Mikunjo hiyo inaweza pia kukusanya bakteria na chembe hai za mwili zilizokufa.

Wakati chembe hizo na bakteria zinapojikusanya katika tezi, askari wa mwili 'chembe hai nyeupe' huanza kazi ya kupambana nazo na pale kazi ya kushambulia inapokwisha hutengeneza vitu vigumu 'mawe' ambayo hubaki ndani ya tezi.

Hata hivyo, baadhi ya watu hujikuta wakimeza mawe pasipo kujua. Iwapo chembe hizo zinaendelea kubaki katikati ya mikunjo ya tezi inazidi kukua na hatimaye kubadilika mawe ya kwenye tezi au 'tonsil stones'.

Hivyo, kladri mawe yanavyoshambuliwa na chembe hai nyeupe au yanapoendelea kubaki katikati ya tezi, inasababisha mtu kusikia maumivu kila mara nyingi anapomeza kitu kama chakula.

Mara nyingi, mawe katika tezi huwapata wenye umri mdogo pamoja na watu wazima wenye tezi 'tonsils' kubwa na wasiozingatia usafi wa kinywa.

Dalili za mawe kwenye tezi ya koo mara nyingi huonekana kama chembe na rangi nyeupe, njano au wakati mwingine kijivu.

Hata hivyo, si mara zote mawe hayo yanaonekana mtu anapofungua kinywa, kwani kuna wakati yanajificha ndani kabisa ya mikunjo ya tezi na kusababisha yasionekane haraka.

Baadhi ya watu hawapati dalili zozote wanapokuwa na mawe kwenye tezi, licha ya viashiria mbalimbali.

Dalili kubwa ya mawe kwenye tezi, ni mtu kutokwa harufu mbaya kinywani ambayo kwa kiasi kikubwa inasababishwa na uwepo wa bakteria waliokaa kwenye mawe hayo.

> Tatu, kuna hatua inayotokea baada ya kutathmini tatizo la mawe kwenye tezi, daktari mhusika anaweza kumshauri mgonjwa afanyiwe upasuaji. Kitaalamu inajulikana kama 'tonsillectomy.'

Dalili nyingine za mawe ya tezi za koo ni pamoja na rangi nyekundu katika sehemu ya tezi kooni.

Pamoja na dalili hizo, kuna waathirika hupatwa na maumivu ya muda mrefu kooni na kuumwa tezi 'tonsillitis' linalojirudia kila mara.

Kuna wakati mtu mwenye mawe kwenye tezi hujisikia kama vile ana kitu kilichomkwama kooni, anachotaka kukimeza, lakini anashindwa.

### MATIBABU YAKE

Mara nyingi mawe ya kwenye tezi, hayana madhara makubwa kwa muathirika, lakini wengi wanapenda yaondolewe kwa sababu ya harufu mbaya kinywani.

Wapo wanaofanya matibabu majumbani na hospitalini. Njia ya kwanza bora ni kuondolewa mawe kwa kutumia kijiti chenye pamba, kwa kuyachokonoa na kuyatoa kwenye tezi yalikojishikiza.

Hivyo mawe yanayoonekana kirahisi pale mtu anapopanua kinywa.

Ni njia inayotakiwa kufanywa kwa umakini mkubwa, kwani tezi ni laini na kukosewa kuna madhara mengine.

Kuna wakati mawe yanajificha, hayaonekani kirahisi. Katika hali kama hiyo, mgonjwa humuona daktari na zaidi kazi humuangukia bingwa wa magonjwa ya masikio, pua na koo (ENT), kufanya huduma ya kutoa matatizo hayo.

Iwapo njia hiyo haitafanikiwa, basi matibabu mbadala hufanyika.

Pili, kuna suala la kusukutua kinywa kwa maji ya chumvi; hiyo inasaidia kusababisha mawe kujachia kwenye kuta za tezi na yanaweza kutoka kirahisi. Ni njia ambayo kwa wenye stadi hiyo kienyeji, hufanyika majumbani.

Tatu, kuna hatua inayotokea baada ya kutathmini tatizo la mawe kwenye tezi, daktari mhusika anaweza kumshauri mgonjwa afanyiwe upasuaji. Kitaalamu, inajulikana kama 'tonsillectomy.'

Hata hivyo, huwa ni uamuzi wa mwisho ambao daktari anatumia, iwapo hali ni mbaya na njia nyinginezo za matibabu zimeshatumika na hazifanikiwa kumaliza tatizo lilopo.

Hata hivyo, ni upasuaji unaoambatana na athari mbalimbali kama vile maumivu makali, kutokwa damu nyingi na madhara mengine ambayo ni lazima yapimwe vizuri katika uzani na daktari, kabla hajaruhusu kufanyika upasuaji.

Baada ya upasuaji wa kuondoa tezi, kasi ya kupona inategemea kiasi cha tezi kilichotolewa, japo kwa wastani mtu huchukua muda kato ya wiki moja na siku 10, kufikia hatua ya kupona kwa usahihi.

### DAWA SAHIHI

Kuna Wakati dawa ya kuua bakteria (antibaiotiki) huweza kutumika kusaidia kuangamiza bakteria washiriki katika kukuza mawe hayo.

Hata hivyo matibabu ya namna hiyo si mazuri, kwa kuwa hayasaidii katika kuondoa mawe hayo au kuondoa kinachosababisha kutokea mawe.

Matibabu hayo, hayapaswi kutumika kwa muda mrefu, kwani inaweza kusababisha kujirudia tatizo hilo.

### MADHARA YAKE

Ni nadra kuona mtu anapata madhara makubwa kutokana na mawe ya tezi. Hata hivyo, orodha ya madhara inajumuisha kuharibika kwa tezi la mgonjwa.

Kuharibika kwa tezi huja pale mtu anapotoa mawe yaliyopo, kwa kutumia vitu kama mswaki na nguvu zaidi inapotumika au kutokuwa umakini, inaumiza tezi husika.

Pia, katika upasuaji kuna wakati inaendana na kutokwa damu nyingi au kupata mashambulizi ya bakteria kwenye kidonda.

Hiyo inazuiwa kwa njia ya kuzingatia usafi wa kinywa. Inashauriwa, usafishaji meno na ulimi kila baada ya mlo, kabla ya kwenda kulala na mara tu baada ya kuamka ni muhimu.

Aidha, kutoa vipande vidogo vya chakula vilivyobaki katikati ya meno kila siku, hali inayosaidia kuondoa uwezekano wa kuwepo bakteria kinywani.

Kuna suala la kusukutua mdomo kila siku kwa kutumia maji maalum, kufanikisha usafi wa mdomo.

Kuna ushauri wa kitabibu kwamba, licha ya kuwapo mbinu nyingi za utaalamu wa afya, njia bora inaangukia katika hali halisi ya tatizo. Upasuaji bado inabaki njia nzuri na sahihi, suluhishi na ya uhakika.

***Mwandishi anapatikna kwa anwani ya baruapepe: jacpole@gmail.com***

MAZINGIRA

SAFARI TANGU 2016

# Bosi Mkuu TFS: Tumenufaika na misitu, vikwazo vyetu hivi...

**Na Elizabeth Zaya**

UNAPOZUNGUMZIWA msitu nchini, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), ndiyo mwenyeji na mwenye wajibu na mamlaka ya kuisimamia misitu hiyo, ikiwamo kuendeleza ustawi wake.

Ni hatua sasa TFS inadokeza historia ya kukumbana na changamoto mbalimbali katika jukumu lake la kulinda misitu, ingawaje sura ya pili ya kujivunia ina mafanikio lukuki yaliyofikiwa, kuendana na matakwa ya Taifa na kimataifa.

Kuna changamoto inayoitaja katika mustakabali wa hifadhi ya misitu, kuhusu suala la uvamizi unaofanywa kwenye hifadhi za misitu katika maeneo mbalimbali nchini, tendo linalochangia uharibifu wa misitu hiyo.

Mtendaji Mkuu wa TFS, Profesa Dos Santos Silayo, anakiri kuwapo tendo hilo, baadhi ya watu kuanzisha makazi ndani ya maeneo ya misitu na kisha yakasajiliwa kama vijiji au vitongoji.

Anasema, ni hali inayochangia kuwapo uharibifu wa misitu kutoka kwa wanavijiji na wageni wanaoingia katika vijiji hivyo.

Profesa Silayo anasema, makazi yanayokuwapo ndani ya hifadhi yanachangia uvunaji haramu wa misitu unaofanywa na wenyeji na wengine kutoka nje ya vijiji, wakifanya kazi hiyo kwa kushirikiana na wanavijiji tajwa.

Sababu nyingine anayotaja inachangia uharibifu katika hifadhi za misitu, pia ni kuwapo mgawanyiko wa usimamizi kati ya serikali kuu na za mitaa.

"Sekta ya misitu inakabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwamo kugawanywa kwa usimamizi wa hifadhi hizo kati ya serikali kuu na serikali za mitaa, jambo linaloleta mwingiliano wa kazi na kupishana kwa vipaumbele vya uhifadhi," anasema Profesa Silayo.

Anatafsiri uwepo wa makazi na vitongoji viliyosajiliwa katika misitu ni uharibifu wa misitu, huku akitaja chanzo kikuu cha uharibifu ni matumizi ya ardhi kupitiliza, akisisitiza "hapo unaweza kuona ni kwa kiasi gani misitu inaharibiwa."

"Vijiji vingi kukosa mipango ya matumizi bora ya ardhi, ufugaji holela wa mifugo ikiwamo kilimo na ufugaji holela wa kuhamahama, ni jambo jingine linalochochea uharibifu wa hifadhi za misitu," anasema Profesa Silayo.

Profesa Silayo anataja lingine ni uchomaji ovyo misitu, jambo waliloamua kulichukulia hatua, kuhakikisha wanakomesha vitendo hivyo kwa nguvu zote.

### MAFANIKIO YALIVYO

Kiongozi huyo mtaaluma anayesimamia misitu ya nchi, anasema wameboresha zaidi usimamizi wa misitu katika kipindi hicho na kwamba, jumla ya hifadhi 455 zimesimamiwa na ziko mpya hekta 104,257 zilizohifadhiwa.



Msitu wa Pori la Akiba, Liparamba, mkoani Ruvuma.

> "Tumefanya mambo mengi mazuri katika kipindi hiki cha miaka mitatu, mchango wa taasisi kwa jamii umeongezeka sana, anasema Profesa Silayo na anawasilisha mfano hao wa mafanikio.




Ofisi ya Pori la Akiba Swaga, iliyoko Kondoa miaka minne iliyopita. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Anaeleza mgawanyiko wake kuna hekta 6,000 za Hifadhi za Nyuki zilizoko Nyasa na Songea Vijijini mkoa wa Ruvuma na Chunya mkoa wa Mbeya, zilizopandishwa hadhi kuwa Misitu ya Hifadhi za Mazingira Asilia, jumla ya idadi zake sasa kufika 12.

Profesa Silayo anadokeza kuwapo hifadhi nyingine nne zilizoko mbioni kutangazwa kuwa misitu ya asili na mingine 89 imeandaliwa mipango bora ya usimamizi.

### UTAJIRI NYUKI

Kuhusu uzalishaji wa mazao ya nyuki, Profesa Silayo anasema umeongezeka, idadi ya asali kutoka tani 15,450 mwaka 2016 hadi tani 34,500 mwaka huu, ambayo ni wastani wa mara mbili na robo ya uzalishaji wa awali.

Pia, anasema uzalishaji wa zao la nta umeongezeka kutoka tani 625 mwaka 2016 hadi 750 mwaka huuu na ongezeko la asilimia 25 na kwamba idadi ya wafanyabiashara wa mazao ya nyuki, imeongezeka kwa asilimia 40.

### MIGOGORO MITI

Profesa Silayo anaeleza kuna mashamba ya hekta 149,950 ya miti yaliyoanzishwa, sasa jumla yake hekta 470,000, yote inalenga kuhifadhi mazingira, kuongeza ajira na mazao ya misitu kwa ajili ya kukodhi mahitaji ya viwanda.

Pia, anasema kuna miche milioni 60 ya miti iliyopandwa katika mashamba na miche milioni 30 inayotolewa na TFS kwa kwa ajili ya kupandwa.

Anasema katika kipindi hicho tangu mwaka 2016, kuna jumla ya migogoro 105 iliyozikabili hifadhi na vijiji katika kipindi hicho cha miaka mitatu, imetatuliwa kwa kiwango kikubwa na kwamba bado wanaendelea kuitatua kuhakikisha inakwisha.

"Katika kutatua migogoro vigingi (beacons) 21,267 kati ya 22,719 imewekwa katika mipaka. Mfano wa migogoro iliyotatuliwa ni Geita, Kasulu, Derema (Muheza), Mkulazi (Morogoro), Pagale, Biharamulo, Iyondo Mswima (Ileje),"anasema Profesa Silayo

### MADUHULI JE?

Profesa Silayo anasema, shilingi bilioni 301 zimeshakusanywa, ikiwa ni ogezeko kubwa kila mwaka, mathalan mwaka wa fedha 2015/16, zilikusanywa Sh. milioni 87.5 na mabadiliko makubwa yanashuhudiwa, katika mwaka wa fedha 2017/18 ikafika Sh. milioni 115.6.

Ni matokeo yanayoendana na maboresho ya makusanyo kwa njia ya elekroniki ambayo ni sehemu ya mageuzi ya mifumo ya kitaifa sasa, tofauti na ilivyokuwa awali.

"Tumefanya mambo mengi mazuri katika kipindi hiki cha miaka mitatu, mchango wa taasisi kwa jamii umeongezeka sana, anasema Profesa Silayo na anawasilisha mfano hao wa mafanikio:

"Kuna jumla ya madawati 20,000 yalitengenezwa na kugawiwa kote nchini, huku mbao zenye thamani ya Sh. milioni 800 zilitolewa kwa halmashauri za wilaya mbalimbali kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa miradi mbalimbali.

"Miradi mingi ya ujenzi wa shule, zahanati, vituo vya polisi na maji imetekelezwa na kwa sasa tunakamilisha mradi wa maji vijiji vya kata ya Ifinga na Madaba, mkoani Ruvuma, ambao utagharimu Sh. milioni 350,' anaeleza.

### VIWANDA VS MSITU

Profesa Silayo anasema, kuna mashamba 11 ya miti yanayovunwa kwa mwaka na yahudumia zaidi ya viwanda 1,000 na anataja kuwapo viwanda vingine zaidi ya 3,000 vinavyohudumiwa na misitu, ikitoa ajira za moja kwa moja kwa watu zaidi ya milioni tatu.

Mkuu hiyo wa TFS anataja mbinu wanayotumia kukabili uvunaji mbaya au usiokubalika wa misitu, mojawapo ni kushirikiana na wananchi jirani kudhibiti, kuvikagua vituo mbalimbali, matumizi ya intelijensia kuzuia uhalifu na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na nchi jirani.



## HABARI DODOMA

# Miradi ya maji 58 kugharimu bil. 4.9/-

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) mkoani Dodoma, umelenga kutekeleza miradi ya maji 58 yenye thamani ya Sh. bilioni 4.986 kwa mwaka ujao wa fedha.

Akizungumza jijini hapa jana, Meneja wa Ruwasa Mkoa wa Dodoma, Dk. Godfrey Mbabaye, alisema miradi hiyo wataitekeleza katika maeneo mbalimbali ya wilaya saba za mkoa huo.

Dk. Mbabaye alisema kuwa kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 2.59 ni kwa ajili ya miradi 28 ambayo ni endelevu, Sh. milioni 345 zimetengwa kwa ajili ya kukarabati miradi 10, Sh. milioni 513 za upanuzi wa miradi na Sh. bilioni 1.5 ni kwa ajili ya ujenzi wa miradi mpya.

"Tunatarajia kutumia zaidi ya Sh. bilioni 4.986 kwa ajili ya kutekeleza miradi 58 kwa mwaka wa fedha ujao, lengo ni kuhakikisha wananchi wanapata maji yaliyo safi na salama ambayo yanakidhi viwango vinavyotakiwa," alisema.

Dk. Mbabaye, akizungumzia utekelezaji wa miradi kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30 mwaka huu, alisema walikuwa wanatekeleza miradi 40 yenye thamani ya Sh. bilioni tisa ambayo hadi sasa mingi imeanza kutoa huduma.

Alisema kati ya miradi hiyo, ipo ambayo haijaanza kutoka maji kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kuharibika kwa miundombinu ya barabara ambayo ilisababishwa na mvua kubwa kunyesha, hivyo kushindwa kufika maeneo ya miradi kwa wakati.

Alisema upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Dodoma ni wa asilimia 62, lakini wanatarajia kufikia Juni 30 mwaka huu, kiwango kitafika asilimia 70.

"Tunatambua kuwa wananchi wanatumia maji yenye magadi katika baadhi ya maeneo, ili kumaliza tatizo hilo, tutavuta maji kutoka Kijiji cha Msisi ili tuyachanganye na yale wanayoyatumia kwa sasa, hii itakuwa suluhisho la tatizo hili kwa wakazi wa Hombolo," alisema.

**"Tunatarajia kutumia zaidi ya Sh. bilioni 4.986 kwa ajili ya kutekeleza miradi 58 kwa mwaka wa fedha ujao, lengo ni kuhakikisha wananchi wanapata maji yaliyo safi na salama ambayo yanakidhi viwango vinavyotakiwa," alisema.**

# Machinga sasa marufuku pembezoni mwa majengo

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

OFISA Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, amewataka wafanyabiashara ndogo (machinga) waliovamia pembezoni mwa majengo ya ofisi na yale yasiyoruhusiwa kufanya biashara, kuondoka kwa maeneo hayo kwa kuwa wanakiuka sheria na kanuni ya Halmashauri ya Jiji.

Yuna alisema hayo jana alipozungumza na viongozi wa wafanyabiashara hao jijini Dodoma, kutokana na baadhi yao kufanya biashara pembezoni mwa majengo ya ofisi kinyume cha kanuni na sheria ya jiji.

Alisema kuna wamachinga wanafanya biashara kwenye maeneo ya pembezoni mwa majengo ya ofisi na kusababisha wafanyakazi wake kutokuwa na utulivu na umakini wa kufanya kazi kutokana na kubugudhiwa.

"Kuna baadhi ya wafanyabiashara wameweka vibanda vya biashara pembezoni mwa majengo ya ofisi mbalimbali ndani ya jiji, hali ambayo imekuwa ikileta usumbufu katika kufanya kazi kwa wafanyakazi wenyewe, hivyo ni lazima wapishe ili wafanye kwa uhuru na usikivu na sivyo vinginevyo," alisema.

Aliwataka viongozi hao wa machinga kuwa mabalozi kwa wenzao ambao wamekuwa wakikiuka sheria kwa kuvamia maeneo kama hayo ya majengo ya ofisi, akiwataka wahakikishe wanatoa elimu, ili waepuke kufanya biashara sehemu zisizoruhusiwa na jiji.

"Uwapo wenu wa viongozi wa machinga ndiyo silaha yangu katika utendaji wa kazi huko mitaani mnakofanya shughuli zenu za biashara, na ndiyo maana hivi sasa hakuna makelele wala migogoro kati yenu na sisi Halmashauri ya Jiji," alisema.

Awali, wakizungumza mbele ya ofisa masoko huyo, viongozi hao walisema kuwa watakuwa tayari kuhakikisha maeneo yasiyo rasmi hayavamiwi ikiwamo kwenye majengo ya ofisi, ili kuondoa usumbufu.

Mwenyekiti wa Machinga Complex 77, Edward Ndahani, amewashauri viongozi wenzake kuisaidia Halmashauri ya Jiji kuondoa mabanda yaliyokaa kwa muda mrefu pasi na kutumika kwa biashara kwa kuwa yanaongeza uchafu jijini.

"Kwenye maeneo yetu tunayosimamia, kuna mabanda ambayo hayafanyi kazi yoyote na yanaonekana ni uchafu, hivyo ninawasihi viongozi wezangu tushirikiane jiji letu katika kuliweka kwenye usafi kwa kuyaondoa mabanda yote yasiyofanya kazi," alisema.

Mwenyekiti wa Machinga Wilaya ya Dodoma, Baraka Marisho, aliwataka wafanyabiashara kushirikiana na Halmashauri ya Jiji kwa lengo la kuondokana na migogoro isiyo ya lazima ikiwamo ya kuvamia maeneo yasiyoruhusiwa.



Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna (katikati), akizungumza na wafanyabiashara ndogo maarufu kama machinga, jijini humo juzi, kuhusu tahadhari ya uvamizi wa maeneo yasiyo rasmi. Kushoto ni Ofisa Msaidizi wa Masoko wa Jiji hilo, Getruda Lumambo na Mwenyekiti wa Umoja wa Wamachinga Wilaya ya Dodoma, Baraka Mrisho. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Majaliwa awapa neno wazee Dodoma maeneo ya kihistoria

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

WAZIRI Mkuu, Kasimu Majaliwa, amewataka wazee wa mkoani Dodoma kwa kushirikiana na viongozi wengine, kuainisha maeneo yote yenye historia ya mkoa huo, ili serikali iyatenge na kuwa maeneo ya vivutio vya utalii.

Alitoa agizo hilo juzi baada ya kupewa taarifa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, kuhusu historia ya eneo la Iyumbu jijini wakati waziri huyo alipowasilisha hotuba kwenye makabidhiano ya nyumba na Shirika la Nyumba (NHC).

Waziri Mkuu aliwata wazee kwa kushirikiana na viongozi wengine kuhakikisha wanaainisha maeneo yote ya kihistoria yaliyoko katika maeneo yao, ili serikali kuangalia yafanyike kuwa maeneo ya utalii.

"Nimeambiwa kuwa hapo eneo karibu na Chuo Kikuu cha St. John ndiyo lenye historia ya Mkoa wa Dodoma, ambapo ilitokana na kuzama kwa tembo na wenyeji wakawa wanapaita kuwa ni Idodomia, sijui tembo alizama mzimamzima au miguu tu, lakini ni muhimu kutunza historia ya maeneo yetu," alisema.

Waziri Mkuu alisema kuwa, baada ya maeneo hayo kuainishwa, wazee hao kwa kushirikiana na viongozi, watakuwa na jukumu la kupeleka hoja hiyo kwenye Baraza la Madiwani la halmashauri husika ili kujadiliwa.

Alisema baraza hilo litakuwa na jukumu la kuyaingiza kwenye mipango na kuyaweka kuwa maeneo ya vivutio vya utalii.

"Tumekuwa tukipata wageni tunawapeleka mbali, kumbe kuna maeneo mazuri yenye historia ya makao makuu yanafaa kuwa vivutio, hakikisheni mnayaainisha haraka, ili tuweze kupata mapato mengine," alisema.

Waziri Simbachawene katika hotuba yake, alimwomba Waziri Mkuu kusaidia kutatua migogoro iliyoko katika maeneo hayo ya kihistoria kutoka na kuvamiwa na watu kwa madai kuwa wamemilikishwa na mamlaka husika.

Simbachawene aliyataja baadhi ya maeneo hayo kuwa ni pamoja Kijiji cha Iyumbu, Mlima wa Mlimwa yaliko makazi ya Waziri Mkuu, eneo la Kikuyu karibu na Chuo cha St. John na Chamwino Ikulu.

"Tumekuwa na shida hiyo muda mrefu na maeneo hayo yamebeba historia ya mkoa wetu wa Dodoma, tunaomba yalindwe ili kuweka kumbukumbu kwa vizazi vyetu vijavyo," alisema.

Nipashe ilifanikiwa kuzungumza na Chifu Lazaro Chihoma anayetunza eneo la matambiko la machifu wa kabila la Wagogo la Bwibwi lililoko Kijiji cha Iyumbu, akiishukuru serikali kwa kuona umuhimu wa kutunzwa kwa maeneo hayo ya kihistoria.

Chifu Chihoma alisema eneo hilo la matambiko lina kisima kirefu ambacho kina historia ya baadhi ya machifu kuzama miaka ya nyuma wakati walipokutana humo ndani ya kisima na kufunikwa na maji kwenye vikao vyao vya kupanga mikakati ya kivita.





# Mil. 80/- kusaidia vita dhidi corona

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAKULIMA wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kupitia kwa mawakala wa pembejeo za kilimo, wamekabidhiwa vifaa vya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Vifaa hivyo ambayo vinathamani ya Sh. milioni 80 vilitolewa juzi na Kampuni ya Uzalishaji Mbolea ya Yara kwa lengo la kuwalinda wakulima dhidi ya corona na kukwamisha shughuli za kilimo.

Akikabidhi msaada huo vikiwamo vitakasa mikono na barakoa Meneja wa Biashara kutoka Kampuni ya Yara, John Rotich, alisema walikusudia kuwalinda wakulima dhidi ya mapambano ya corona.

"Kwa kutambua umuhimu wa wateja wetu ambao ni wakulima tuliamua kununulia vifaa vya kujikinga na corona vyenye thamani ya shilingi milioni 80 naamini vitaongeza nguvi kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa huo na wakulima kuendelea na shughuli za uzalishaji kama kawaida," alisema Rotich.

Mwakilishi wa mawakala wa wakulima Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Olaisi Olesenga, aliishukuru kampuni hiyo kwa kulikumbuka kundi hilo, kuwapatia msaada wa vifaa vya kujikinga.

Lakini aliipongeza serikali kwa kutozuia watu kutoka majumbani wakati wa janga la corona kwa maelezo kuwa endapo ingefanyika hivyo mazao mengi ya wakulima yangeharibika mashambani.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa niaba ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Ofisa Uchumi na Uzalishaji, Juma Madito, aliwataka wakulima kutunza na kuongeza uzalishaji wa mazao katika kipindi ambacho dunia inakabiliwa na janga la corona.

Alisema baada ya madai ya muda mfupi maneno mengi yakiwamo ya nchi jirani yatakumbwa na uhaba wa chakula na wao tutawauzia kwa fidia.

**"Kwa kutambua umuhimu wa wateja wetu ambao ni wakulima tuliamua kununulia vifaa vya kujikinga na corona vyenye thamani ya shilingi milioni 80 naamini vitaongeza nguvi kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa huo na wakulima kuendelea na shughuli za uzalishaji kama kawaida," alisema Rotich.**

# Walalamika kulipa maelfu kutibiwa hospitali ya wilaya

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

WAKAZI wa Kijiji cha Madundasi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, wamesema wanalazimika kulipa nauli ya Sh. 400,000 kwa bodaboda kama gharama ya usafiri kwa wagonjwa kuwapeleka Hospitali ya Wilaya ya Chunya kutokana na tatizo la miundombinu ya barabara kutopitika kwa urahisi.

Wakizungumza na Nipashe jana kijijini hapo, walisema sababu inayochangia gharama kubwa ni kutokana na barabara zinazounganisha kijiji hicho kujaa maji, hivyo kutopitika.

Mwenyekiti wa Kijiji, Seni Lelesi, alisema yeye ni miongoni mwa watu waliolazimika kulipa gharama ya Sh. 400,000 kumpeleka mwanawe hospitali kujifungua.

Alisema kutokana na tatizo la barabara mjukuu wake alifia tumboni kutokana na ubovu wa barabara wakiwa njiani kuelekea Hospitali ya Wilaya ya Chunya.

Tatizo la barabara ni kubwa hapa kijiji cha Madundasi, mimi mwenyewe ni mwathirika nilimpoteza mjukuu wangu, lakini namshukuru Mungu mwanangu walimwokoa, tumeshuhudia watu wengi wakipoteza maisha kutokana na ubovu wa barabara," alisema Lelesi.

Tatu Shinamwalenga alisema mwezi Februari mwaka huu alishuhudia mama akipoteza maisha akiwa kwenye bodaboda kuelekea Chunya kutibiwa.

Alisema alitumia shilingi 400,000 yeye pamoja na nesi na kwamba alipofia njiani alirudishwa tena kwa gharama ya shilingi 400,000.

Alisema barabara ni shida kwani hata wafanyabiashara wanalazimika gharama ya shilingi 5,000 kufuata huduma Kata ya Igurusi na kuuza bidhaa zao kwa gharama kubwa.

Zengo Zengo, alisema usafiri pekee unaotegemewa kijijini hapo ni bodaboda, na kwamba kipindi cha masika hawawezi kusafiri kabisa kwenda eneo lingine, kutokana na mawasiliano ya barabara ndani ya kijiji hicho kutopitika kwa sababu ya mito kujaa maji na mafuriko.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Ismail Chungu, alikiri kuwapo kwa changamoto ya barabara na kwamba hata yeye alishindwa kushiriki vikao vya maendeleo ya kata.

Alisema kipindi cha masika jumla ya watu wanne walipoteza maisha wakiwamo wajawazito wawili na wagonjwa wa kawaida wawili wakati wakipelekwa Hospitali ya Wilaya ya Chunya.

Aliongeza kuwa uongozi wa wilaya unafahamu tatizo la barabara katika kijiji hicho na kwamba wanashindwa hata kuwatembelea kutokana na kadhia hiyo.



Waendesha bodaboda wakipita kwa tabu baada ya mawasiliano ya barabara inayounganisha vijiji vya Luhanga na Madundasi katika Kata ya Luhanga, Halmashauri ya Mbarali, mkoani Mbeya, kukatika kutokana na maji kujaa jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Jela miaka saba kwa wizi wa mali

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya imemhukumu kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka saba jela Joseph Simon, mkazi wa Forest baada ya kukutwa na hatia ya wizi wa mali zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni mbili.

Hukumu hiyo ilisomwa juzi na Hakimu, Andrew Scout baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili katika kesi hiyo.

Hakimu Scout alisema alimtia hatiani mshtakiwa Joseph Simon (Kipesa) baada ya kueleza kuridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka akidaiwa kuiba kompyuta mpakato mbili kinyume na kifungu namba 258 (1) & 265 na kumwachia huru aliyekuwa mshtakiwa wa pili, Gabriel Mwandwanga, baada ya Jamuhuri kushindwa kuthibitisha shtaka dhidi yake akidaiwa kupokea mali ya wizi kinyume na kifungu namba 311 cha sheria ya kanuni ya adhabu.

Hakimu huyo alisema ushahidi wa Jamuhuri kupitia mashahidi saba ulithibitisha kwamba Machi, 2019, katika eneo la Forest mshtakiwa Simon alivizia gari la mlalamikaji Elias Jengela aliyepaki gari lake nje ya nyumba yake na baada ya kutoka alikuta gari lake limevunjwa kioo cha nyuma na kuibiwa mfuko uliokuwa na kompyuta mpakato mbili na chaja zake vyenye thamani ya Sh. milioni 2.2.

Baada ya mshtakiwa kutiwa hatiani aliomba mahakama kumpunguzia adhabu, huku mwendesha mashtaka wa serikali, Wakili Baraka Mgaya, aliomba mahakama kutoa adhabu kali akisema matukio hayo yamekuwa mengi mitaani ndipo Hakimu Scout aliamuru mtu huyo kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka saba.


Wakati huo huo, mahakama hiyo ilimwachia huru Brithon Ndibize aliyekuwa mgombea uenyekiti wa Serikali ya Mitaa wa Kati katika Kata ya Ruanda kupitia Chadema baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha shtaka dhidi yake la kutishia kuchoma ofisi za serikali.

Upande wa mashtaka ulikuwa ukidai kwamba wakati wa mchakato wa kuchukua na kurudisha fomu za kugombea uenyekiti serikali za mitaa, mtu huyo alitoa kauli ya kutishia akiinukuu kwamba 'leo lazima kieleweke, nyie watendaji dawa yenu ni ndogo, dawa yenu nitachoma ofisi yangu na ya kata tuone hizo kazi mtafanyia wapi' mwisho wa kunukuu kauli mojawapo inayodaiwa kutolewa na Mwanachadema huyo baada ya kuenguliwa kuwa mgombea baada ya kukosea ujazaji fomu.

Baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili, hakimu huyo alisema upande wa mashtaka ulikuwa na jukumu la kuthibitisha bila kuacha shaka yoyote shtaka la kutishia, ingawa haoni kama kulikuwa na tishio, pia mshtakiwa kutochukuliwa hatua na wananchi waliokuwa ofisi ya mtaa kama kweli kulikuwa na tukio la kutishia amani, kati ya wagombea 11 wa Chadema mmoja pekee kudaiwa kutishia.

Mengine ni kutokuwapo na mtu aliyepinga kwamba mshtakiwa hakuridhika na mchakato wa uchaguzi huo, ndio maana akaenda kupeleka barua ofisi ya mtaa na baada ya kutopokelewa aliienda kwa Ofisa Mtendaji wa Kata ndipo akiwa njiani alikamatwa baada ya kata kushauriwa na Mkurugenzi wa Jiji mambo yaliyoelezwa na mahakama kutia shaka katika ushahidi wa Jamhuri.

Kufuatia upungufu huo, hakimu akaona shaka na kumwachia huru mshtakiwa Brithon Ndibize chini ya kifungu namba 89 (2) a na b na kifungu namba 235 (1) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu.



## Tamwa yaasa wajasiriamali kutokata tamaa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKURUGENZI wa Chama cha wanahabari wanawake Tanzania (Tamwa), upande wa Zanzibar, Dk. Mzuri Issa amewataka wajasiriamli kutokata tamaa licha ya changamoto katika harakati zao za uzalishaji wa bidhaa.

Dk. Mzuri aliyasema hayo wakati wa ziara maalumu ya kutembelea vikundi katika shehia mbalimbali za Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa lengo la kujionea namna wajasiriamali wanafanyia kazi elimu wanayopewa kupitia chama hicho.

Aliwataka wajasiriamali hao kutokata tamaa licha ya changamoto walizonazo ikiwamo ya ukosefu wa huduma ya maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Alisema kuna jitihada kubwa zimefanywa na wajasiriamali na wanapaswa kuungwa mkono kwa kuwa lengo lao ni kujikwamua na umaskini.

Pia, alisema Tamwa-Zanzibar itaendelea kufanya kila jitihada zenye lengo la kuhakikisha wanawasaidia wajasiriamali hao ili waweze kutimiza ndoto zao.

Katika hatua nyingine aliwataka wanawake kuzitumia fursa mbalimbali kwenye jamii ikiwamo za kushiriki katika harakati za uchaguzi kugombea nafasi za kisiasa.

Aliwataka wanawake hao kuacha kubweteka na kudhani nafasi za uongozi ni za wanaume pekee badala yake wanapaswa kujitambua na kuwa tayari muda wowote.

Naye Ofisa uwezeshaji wanawake kiuchumi Tamwa-Zanzibar, Nairat Abdalla, aliwataka wajasiriamali hao kutoridhika na masoko ya bidhaa zao kwenye maeneo husika na kubuni njia zingine mbadala.

Alisema kuna fursa nyingi za masoko kupitia bidhaa hizo hivyo ni vyema kuyatumia masoko hayo ili waweze kujingizia kipato zaidi.

Kwa upande wao wajasiriamali hao walisema wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maji kwa ajili ya kuendeleza kilimo.

"Tungekuwa na maji ya kutosha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji tusingelalamika na ugumu wa maisha kwa sababu kilimo kina faida kubwa, lakini tatizo letu ni maji," alisema Rehema Abasi kutoka Kijiji cha Bubwini.

**Alisema kuna jitihada kubwa zimefanywa na wajasiriamali na wanapaswa kungwa mkono kwa kuwa lengo lao ni kujikwamua na umaskini.**

# ZEC: Tusibebeshwe lawama Daftari la mpigakura

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KUTOKANA na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi kukosa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi Kisiwani Pemba na kukosa kujiandikisha katika Daftari la Wapigakura, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji mstaafu Hamid Mohamoud Hamid, amesema Tume hiyo haiwezi kubeba lawama kwa wananchi kukosa vitambulisho hivyo.

Alisema wanaohusika kutoka vitambulisho hivyo ni mamlaka nyengine na Tume yake haihusiki na kwamba bila ya kutokuwa na kitambulisho hicho mtu hawezi kuhakikiwa wala kuandikishwa katika daftari la wapigakura.

Akizungumza na Waandishi wa habari Kisiwani Pemba, alieleza kuwa kazi ya Tume hiyo ni kuandikisha wapigakura wapya na uhakiki wa wapigakura waliomo katika Daftari la kudumu la wapigakura wakiwa na sifa zinazostahiki.

Alisema ZEC inafanya kazi zake kwa mujibu wa Sheria za Zanzibar na haiwezi kwenda kinyume na sheria hiyo, hivyo inaandikisha wapigakura kwa mwananchi yeyote ambaye anakitambulisho kipya cha Mzanzibar mkaazi alichokipata kutoka mamlaka husika.

Alieleza kuwa ZEC, haijamzuia mwananchi yeyote kujiandikisha ama kuhakiki taarifa zake iwapo atakuwa na kitambulisho hicho.

"Kitambulisho cha Mzanzibar mkaazi hakitolewi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar wala ZEC haina mamlaka hiyo," alisema.

Akizungumzia suala la uandikishaji wapigakura wapya na uhakiki wa taarifa za wapiga kura wapya, alisema Tume hiyo imefanya marejeo ya zoezi hilo kama ilivyowaahidi wananchi kwa nia ya kumtaka kila mwenye sifa aweze kujiandikisha.

Alisema Tume ilitoa fursa kwa mara ya pili kwa kuwaheshimu wale waliokosa kujiandikisha mara ya kwanza kwa ajili ya kukosa vitambulisho na ilitoa muda wa kutosha wa kutafuta vitambulisho kwa kuwa inafanya kazi muda maalumu.

Alisema ZEC, ina muda maalumu wa kufanya kazi zake ikiwamo kusajili wapigakura na uhakiki wa taarifa za wapigakura waliomo katika Daftari la kudumu la wapigakura kwa ajili ya matayarisho ya uchaguzi mkuu, hivyo usajili huo ni maandalizi ya uchaguzi huo.

Akielezea usajili wa wapigakura wapya uliokwenda sambamba na hakiki wa taarifa za wapigakura waliomo kwenye Daftari la kudumu lililofanyika Kisiwani Pemba, alisema lilikwenda vyema huku amani na utulivu ikitawala katika maeneo yote ya uandikishaji.

Alisema mwitiko ulikuwa mkubwa kwa wale wenye vitambulisho ambavyo vinatakiwa na Sheria ya Uchaguzi walijitokeza kutumia fursa yao hiyo ya kujiandikisha ili waweze kuwa wapigakura kwa uchaguzi mkuu muda utakapowadia.

Uandikishaji wapigakura wapya na uhakiki wa wapigakura waliomo kwenye Daftari la kudumu la wapigakura kisiwani Pemba umemalizika na unatarajiwa kuanza kwa mara ya pili kisiwani Unguja Juni 5.



Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa (mbele), akiwa katika ziara ya kukagua eneo ambalo linatarajiwa kulimwa kilimo cha mboga, kijiji cha Kidoti, Mkoa wa Kaskazini Unguja juzi, ikiwa ni harakati za kuwasaidia wanawake wa kijiji hicho, ili waweze kujikwamua kiuchumi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali kupeleka boti 5 visiwa vidogo Unguja, Pemba

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema itanunua boti tano kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wanaoishi katika visiwa vidogo vilivyopo Unguja na Pemba.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji, Dk. Sira Ubwa Mamboya, wakati akiwasilisha makadirio, mapato na matumizi ya bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2020-2012, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema hiyo ni ahadi ya Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein ya kuona wananchi wanaoishi katika visiwa vidogo wanapata huduma za usafiri wa uhakika wakati wanapovuka bahari kuelekea upande wa pili.

Dk. Mamboya alisema ujenzi wa boti hizo umeanza ukifanywa na kampuni ya Damen Shipyards kutoka Uholanzi na hadi kufikia Machi 2020, kazi hiyo imefikia asilimia 65.

"Mheshimiwa Spika napenda kulijulisha Baraza la Wawakilishi kwamba kazi ya ujenzi wa boti tano kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri kwa wananchi wanaoishi katika visiwa vidogo vidogo umeanza na umefikia asilimia 65," alisema.

Alisema boti hizo zitatumika kwa wananchi wanaoishi katika kisiwa cha Tumbatu, Mkoa wa Kaskazini Unguja chenye wakazi wapatao 45,000, ambao hadi sasa huduma za usafiri wa kwenda upande wa pili wa bandari ya Mkokotoni hutumia boti zinazomilikiwa na watu binafsi.

Vile vile, alisema boti hizo zinatarajiwa kupelekwa katika kisiwa cha Fundo, Kojani, Kisiwapanza pamoja na Makoongwe kwa upande wa Pemba na kwa kawaida wananchi wa visiwa hivyo walikuwa hawana huduma za usafiri wa uhakika.

Baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walifurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuwatafutia wananchi wake usafiri wa uhakika wa boti kwa lengo la kuepusha matukio makubwa ya ajali.

Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake Pemba, Suleiman Sarhani, alimpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein kwa juhudi zake za kuhakikisha wananchi wanaoishi katika visiwa vidogo wanapata huduma za usafiri wa uhakika.

"Tunampongeza kwa dhati Dk. Shein kwa juhudi zake za kuona wananchi wanaoishi katika visiwa vidogo wanapata huduma za uhakika za usafiri kwa kuwapatia boti zenye uwezo wa kutoa ufanisi mkubwa," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**ABA-JAJA COMPANY LIMITED**

| S/N | MAHAKAMA | WADAAWA | MALI INAYOUZWA | TAREHE NA MUDA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO SHINYANGA | AFRISIAN GINNERY CO.LTD Dhidi ya MAISHA DOMINIC KILOMBA | NYUMBA MOJA IPO MHONGOLO KAHAMA | 30/6/2020 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI |

**MASHARTI;**

1. Mnada unafanyika eneo la Mhongolo Kahama mahala nyumba ilipo.
2. Mnunuzi atalipa 25% ya bei aliyofikia na 75% ndani ya siku 14 Baada ya siku ya mnada.
3. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**KWA MAWASILIANO**
**ABAJAJA CO.LTD AND COURT BROKER**
**BOX 565, SHINYANGA**
**SIMU; 0786652286/ 0754652268/ 0622652268**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **Talib Hussein Talib** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 655 CJG** TOYOTA MARK 2. Rangi- pearty white. Chassis No. **GX 1100010635.** Engine No. **1GFE7412588.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/424258/2020.**

115761802

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**WINFRIDA MPAGAMA ALPHANIES** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 427 CKU.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **MBE/MBE/RB/83256/2020.**

115761402

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GODFREY SHIJA SHIJA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 847 AVN** AINA YA SUZUKI ESCUDO. KWA YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI **KAH/TR/RB/203/2020.**

115761502

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
Tarehe 04-06-2020

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe **05-06-2020** kampuni ya **ESTIM CONSTRUCTION CO. LTD** itasafirisha Mzigo Excavator Machine wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar es salaam kuelekea Dodoma kupitia barabara ya Morogoro.** Gari hilo lenye namba za usajili:

   **T 296 BWN / T 106 AYZ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

   Urefu - mita 20.00
   Upana - mita 3.0
   Kimo - mita 4.8

3. Njia itakayotumika: **Dar es salaam hadi Dodoma kupitia barabara ya Morogoro.**

   Magari yatasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115761602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ZAINAB INAYAT ALI KARAMALI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 502 BHZ** TOYOTA CHASER. Chassis No. **GX1000114968.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/SEL/RB/408336/2020.**

115761902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Anaitwa **YAIRO G. MSIGALA** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajiri **T 297 DME** aina yake **ZHONGTONG BUS** yenye engine namba **78522271** na chassis namba **LDY4GL2B1HOOO9773.** Kwa yeyote atakeiona anaombwa atoe taarifa ktk kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MOR/MOR/RB/417685/2020.**

115761102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO KARIAKOO**

**MADAI YA TALAKA NO. 18/2020**

**POPOTE ULIPO**

**NDUGU SHITALBEN RAMANBHAI PARMAR WA INDIA**

**MADAI YA TALAKA NO. 18/2020**

**MDAI: DHARMENDRA MADHAW GAIKWAO**

**MDAIWA: SHITALBEN RAMANBHAI PARMAR**

Mtajwa hapo juu unaamuriwa na Mahakam hii kuja kusikiliza shauri lililotajwa hapo juu siku ya JUMATATU tarehe 22/6/2020 saa 2.30 asubuhi bila kukosa na kama hukuhudhuria shauri hili litasikilizwa upande mmoja.

Amri hii inatolewa kwa amri yangu leo tarehe 02/06/2020.

HAKIMU

MAHAKAMA YA MWANZO KARIAKOO
DAR ES SALAAM

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO
KARIAKOO - ILALA
DAR-ES-SALAAM

115761202

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# Meneja bandari amtunishia misuli DC

**Na Ashton Balaigwa,**
BAGAMOYO

MENEJA wa Mamlaka ya Bandari ndogo iliyopo wilayani Bagamoyo mkoani Pwani,Witharo Jared, 'ametunishiana misuli' na Mkuu wa wilaya hiyo, Zainab Kawawa, alipotakiwa kutoa sababu za kushuka kwa mapato katika bandari hiyo pamoja na malalamiko ya wafanyabiashara.

Tafrani hiyo ilitokea katika kikao kilichoitishwa na Mkuu wa wilaya hiyo, kikijumuisha wafanyabiashara, Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Mapato Tanzania(TRA),Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania(TAEC) na Maofisa wa Forodha.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkuu huyo wa wilaya ya Bagamoyo, alisema amebaini mapato kushuka katika bandari hiyo kutoka Sh. bilioni tatu Novemba mwaka 2019 hadi Sh. milioni 293.8 Mei, mwaka huu kiwango ambacho alisema kimetishia uchumi wa wilaya hiyo.

Hata hivyo, mkuu huyo wa wilaya alisema kuwa katika uchunguzi aliofanya amegundua sababu mojawapo ya kushuka kwa mapato hayo ni pamoja wafanyabiashara katika wilaya hiyo kuihama bandari katika kupitisha mizigo yao.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Peter Mongi, alisema sababu ya kuhama bandari ya Bagamoyo na kukimbilia bandari ya Mbweni iliyopo wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam ni meneja wa bandari hiyo kuwatolea lugha chafu, kuwadhalilisha na kuwakadilia ushuru tofauti na wanapohoji wanaambiwa wana uamuzi ya kutumia bandari hiyo au kuacha.

"Mkuu wa wilaya kuna mengi yanatusibu, hatujui makadirio ya ushuru, wakati mwingine unapokuwa na mzigo wa madumu 1,000 ya mafuta ya kula anakutajia ushuru wa milioni moja, ukilipia na kudai risiti anakupa ya Sh. 200,000, ukimhoji inakuwaje anakutishia kukupiga au anakwambia nenda sehemu nyingine," alisema Mongi.

Mfanyabiashara mwingine, Chikumba Osward, alimueleza mkuu huyo wa wilaya kuwa kilichowashinda kutumia bandari ya Bagamoyo licha ya kulipa kodi wamekuwa wakitukanwa matusi na dharau kutoka kwa wanayemlipa kodi na hivyo wameamua kuacha na kukimbilia sehemu nyingine.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara hao, Shabani Hamsini, alithibitisha madai hayo na kueleza kuwa kero hiyo imesababisha ugumu wa biashara kutokana na baadhi kuingiza bidhaa bila kulipa kwa kutumia bandari zingine.

Baada ya wafanyabiashara hao kuwasilisha malalamiko hayo, Mkuu wa wilaya hiyo, alimtaka meneja huyo wa TPA kujibu malalamiko hayo ikiwamo manyanyaso, lugha chafu na utaratibu mbovu wa malipo ya mizigo.

Akijibu malalamiko hayo, Meneja huyo alisema wafanyabiashara hao hawajalazimishwa kutumia bandari hiyo na wanaweza kutumia nyingine ambazo zinawapa faida kauli ambayo ilimchefua mkuu huyo wa wilaya na kumtaka akae chini.

Mkuu huyo wa wilaya aliendelea kumhoji kuhusu mikakati ya bandari na changamoto zinazoikabili bandari hiyo ikiwamo uchafu na kufanya maboresho na hatua zilizochukuliwa kuhusu kupandisha mapato yaliyoshuka kwa kiwango kikubwa.

Meneja huyo wa TPA aliposimama kujibu hoja ya mkuu huyo wa wilaya, alimwambia mkuu huyo wa wilaya hapaswi kutoa taarifa kwake zinazohusu bandari bali zinakwenda moja kwa moja makao makuu, hatua ambayo iliendelea kumkasirisha mkuu huyo wa wilaya na kutaka apelekewe huo muongozo unaokatazwa kuwa Mkuu wa Wilaya hapaswi kujua shughuli za bandari.

"Yani mimi mkuu wa wilaya ya Bagamoyo sina mamlaka ya kupata taarifa inayohusu hii bandari hata kopi tu?, mbona taasisi zingine zinaleta taarifa kwangu hapa, kwa kauli yako hiyo umeidharau kamati yangu yote ya ulinzi na usalama," alisema Kawawa na kuongeza:

"Sasa nataka kuona huo muongozo, unasema hicho kitu na nijue mimi na Mkurugenzi wako wa TPA nani mkubwa katika wilaya hii, kama sitapata huo mwongozo namuagiza OCD akuweke ndani" alisema Kawawa.

Kawawa aliagiza vyombo vya ulinzi na usalama vya wilaya hiyo kuchunguza tuhuma zilizotolewa na wafanyabiashara hao dhidi ya meneja huyo wa bandari ya Bagamoyo na ikibainika ni kweli hatua zaidi zichukuliwe dhidi yake.

## RC amtaka DC kurejeshwa mil.150/- zilizopotea

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, ametoa siku saba kwa wahusika waliokuwa wakikusanya mapato kwa njia ya mashine za posi na kushindwa kuwasilisha fedha zaidi ya shilingi milioni 150 kwa Halmashauri ya Mkuranga.

Mhandisi Ndikilo alitoa agizo hilo jana wakati wa baraza maalumu la kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Ndikilo alimtaka pia Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filbato Sanga, kumpatia majina ya waliohusika na ukusanyaji wa mapato na kushindwa kuwasilisha fedha hizo halmashauri.

"Hata kama ni mtumishi wa serikali lazima irudishe fedha zetu, Mkuu wa Wilaya anipatie majina ya wale waliokuwa wakihusika na kukusanya mapato kwa njia ya posi," alisema.

Ndikilo alisema baadhi ya watumishi wa halmashauri waliosababisha hasara ya shilingi milioni 150.3 za mapato, lakini hazifikishwa halmashauri na hivyo kusababisha kufunguliwa kesi mahakamani.

Alisema, wahusika wanatakiwa kurejesha fedha hizo, huku hatua za kisheria dhidi yao zikiendelea kuchukuliwa lengo kutoa fundisho kwa wengine.

Mkuu huyo wa Mkoa alitoa wito kwa Mkurugenzi na Baraza la Madiwani kuepuka kutoa mikataba mibovu kwa mawakala wa ukusanyaji wa mapato.




Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela (wa pili kulia), akijadiliana jambo na baadhi ya madiwani, baada ya kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo, jana. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Godwin Gondwe. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

## Serikali kufanya msako wa sukari Dar

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema itafanya msako jijini Dar es Salaam kwa wafanyabiashara wote ambao wanauza sukari kinyume cha bei elekezi iliyopangwa ya Sh. 2,600 mkoani humo.

Hatua hiyo inakuja baada ya kupokea malalamiko kutoka wananchi ya baadhi ya wafanyabiashara kuuza bidhaa hiyo kwa bei ya juu.

Katika mahojiano na gazeti hili Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema licha ya serikali kutoa maelekezo ya bei elekezi ya sukari, baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakiiuza kwa bei ya juu wakati hakuna upungufu wa bidhaa hiyo.

Alisema bei elekezi iliyotolewa na serikali itabaki kuwa angalizo kwa wafanyabiashara ambao wanatumia kama fursa kujipatia faida kubwa.

"Kutokana na hali hii, ni vyema kwa sasa kwenda duka kwa duka ili kuwakamata wafanyabiashara wote ambao wanauza sukari kwa bei ya juu wakati serikali ilishatoa maelekezo ya bei elekezi.

"Tutachukua hatua dhidi ya wafanyabiashara ambao tutawakuta wamekiuka sheria na taratibu za nchi, hatutanii, inaonekana bado kuna wafanyabiashara ambao wanapata faida mara mbili."

Nipashe ilizunguka maeneo tofauti jijini Dar es Salaam na kubaini maduka mbalimbali yakiuza bidhaa hiyo kati ya Sh. 3,000 hadi Sh. 4,000, ambapo baadhi ya wakazi walisema uhaba wa sukari na bei kubwa imewaathiri sana na hawawezi kukidhi gharama hiyo na kuiomba serikali kuitatua.

Grace Msuya, mfanyabiashara wa jumla Mbezi Luis, alisema kuna muda anatumia siku mbili kuipata bidhaa hiyo kutokana na uhaba.

# LAMPARD HESABU ZAKE KWA SANCHO, COUTINHO



**LONDON,** England

FRANK Lampard ameripotiwa kutaka kuwasajili Jadon Sancho na Philippe Coutinho kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chake cha Chelsea.

Kocha huyo wa The Blues hao anataka kufanya maboresho kwenye kikosi chake baada ya kupita madirisha mawili ya usajili bila ya kunasa staa mpya, huku hivi karibuni wakifanikiwa kumnasa winga wa Ajax, Hakim Ziyech pekee.

Kwa sasa ataendelea kubaki na wachezaji wake makinda wakati msimu wa Ligi Kuu England utakapoendelea, lakini mara utakapokwisha tu na dirisha la usajili kufunguliwa basi atahitaji sura mpya chache kwenye chama lake hilo.

Lakini, kuhusu Sancho, wapinzani wao Manchester United ndio wanaonekana kuongoza kwenye mbio za kumsajili Mwingereza huyo, hivyo wanafahamu itakuwa shughuli pevu kwenye mapambano hayo, huku suala la Coutinho nalo likiwa na upinzani mkali kutokana na Arsenal kuonekana kuhitaji huduma yake pia.

Sura nyingine mpya anazozisaka Lampard ni beki wa kushoto wa Leicester City, Ben Chilwell, ambaye anaweza kumgharimu Pauni 60 milioni, kiungo mshambuliaji wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz na straika wa RB Leipzig, Timo Werner.

Golini, kutokana na kipa Kepa Arrizabalaga kuwa kwenye mashaka makubwa huko Stamford Bridge, Roman Burki wa Borussia Dortmund sasa anapigiwa hesabu na Lampard.



# Solskjaer ajitosa kumuwania Kai

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer ameripotiwa kuingia kwenye mbio za kufukuzia huduma ya mchezaji wa Ujerumani, Kai Havertz.

Manchester United wanamtazama nyota huyo wa Bayer Leverkusen kuwa ni mwenye kipaji cha kutosha cha kwenda kucheza kwenye kikosi chao wakiamini kwamba atakuwa mchezaji wa daraja la juu sana siku chache zijazo.

Kocha Solskjaer ametajwa kumuwania mkali wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, ambaye wikendi iliyopita alifunga 'hat-trick' yake ya kwanza, wakati timu yake ilipoichapa Paderborn 6-1 kwenye Bundesliga.

Mpango namba moja ni kumsajili Sancho, lakini baada ya hapo watamnasa pia Havertz, ambaye wanaamini wasipofanya hivyo mwaka huu basi thamani yake itakuwa kubwa zaidi mwakani.

Kwa kuanzia, Man United imepeleka ofa ya pauni milioni 50 ya kunasa saini ya Havertz, huku wakiamini mkwanja huo utatosha kabisa kwenye kupata huduma ya mchezaji huyo wanayemsaka kwa nguvu zote.

Havertz amekuwa akiwindwa na vigogo msimu huu baada ya kufunga mabao 15 katika michuano yote. Man United wameshafahamu watamtumiaje, ikiwa ni pamoja na kumchezesha kwenye wingi moja au akitokea kwenye kiungo cha kati.

# Marchisio atumaini Ronaldo kubaki Juve

**TURIN,** Italia

CLAUDIO Marchisio ana matumaini nyota wa Juventus, Cristiano Ronaldo atabaki kwa miamba hao wa Serie A, huku uvumi ukienea kwamba kuna uwezekano akaondoka.

Ronaldo alitua Juve akitokea Real Madrid kwa ada ya euro milioni 100 mwaka 2018 na mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or aliisaidia kubeba taji la Ligi Kuu katika msimu wake wa kwanza.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 35, amefunga mabao 21 kwenye Serie A katika mechi 22 alizocheza msimu huu na 25 katika mashindano yote kabla ya ligi kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, huku Juve wakiongoza ligi kwa tofauti ya pointi moja.

Kumekuwa na uvumi kwamba, nahodha huyo wa Ureno anaweza kuondoka hapo Turin na kwenda kwa miamba wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Paris Saint-Germain, huku akihusishwa na klabu yake ya zamani.

Marchisio ambaye aliondoka Juve na kwenda Zenit mwaka 2018 kabla ya kustaafu soka mwaka uliofuata, aliulizwa kuhusu Ronaldo na alisema kupitia mahojiano ya Instagram: "Kabla hajasaini Juve tulikutana mara nyingi. Kwa uhakika anakuweka kwenye wakati mgumu kucheza dhidi yake.

"Kwamba ataondoka? Sijui, lakini nina matumaini hataondoka. Ameshajiimarisha mwenyewe pale Juventus na sidhani kama ana mpango wa kuondoka."



# CRESPO: MARTINEZ ACHANA NA BARCA




**BUENOS AIRES,** Argentina

HERNAN Crespo amemtaja Lautaro Martinez kama "mchezaji aliyekamilika" na amemtaka mshambuliaji huyo kuitosa Barcelona na kubakia Inter Milan.

Martinez mwenye umri wa miaka 22, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia kwa mabingwa hao wa LaLiga baada ya kuwa na msimu wa kuvutia pale Inter, akifunga mabao 16 katika mechi 31 msimu huu wa 2019-20.

Mshambuliaji wa zamani wa Inter na Argentina, Crespo anaamini Martinez anatakiwa kubaki San Siro na kujiimarisha yeye mwenyewe zaidi kabla ya kuondoka.

"Ningependa yeye abaki Inter kwa sababu huu umekuwa mwaka wake wa kwanza," alisema akinukuliwa na David de las Heras kwenye YouTube, kupitia Sport.

"Nataka ajijengee kwanza msingi imara kabla ya kuangalia kubadili timu. Kwani naamini yeye ni mmoja wa wachezaji aliyekamilika kabisa."

Crespo, ambaye kwa sasa ni kocha mkuu wa timu ya Defensa ya Justicia, alishinda mataji matatu ya Serie A akiwa na Inter, ambapo mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea alikaa misimu minne katika klabu hiyo.

Akiwa na umri wa miaka 44 sasa, anataka kumuona Martinez, ambaye ana mabao tisa kwenye timu ya Taifa ya Argentina katika mechi 17, kuendelea kubakia hapo.

## Thiago arudi rasmi mazoezini Bayern

**MUNICH,** Ujerumani

THIAGO Alcantara amerudi kwenye mazoezi baada ya kukosa michezo mitatu ya Bayern Munich kutokana na kuwa majeruhi.

Kiungo huyo alikaa nje katika mechi za ushindi za Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, dhidi ya Eintracht Frankfurt, Borussia Dortmund na Fortuna Dusseldorf kutokana na matatizo ya maumivu ya nyama za paja.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania alirudi kwenye mazoezi Jumanne na sasa anajiandaa kucheza dhidi ya Bayer Leverkusen Jumamosi.

Lucas Hernandez, ambaye aliumia wakati wa mchezo wa ushindi wa 5-0 dhidi ya Dusseldorf, anaweza pia kuanza mazoezi ya peke yake, huku majeruhi wengine, Niklas Sule na Philippe Coutinho wakiendelea kujiuguza.

Ushindi wa Bayern katika mchezo huo wa Jumamosi pale katika dimba la BayArena unaweza kuwa nafasi nzuri zaidi ya kulikaribia taji la Ligi Kuu.

Kikosi hicho cha kocha, Hansi Flick kinaongoza kwa tofauti ya pointi saba kileleni dhidi ya Dortmund waliopo nafasi ya pili, huku zikiwa zimebakia mechi tano ligi kumalizika.



## *Jorginho hajawasiliana na Juventus - Wakala*

**TURIN,** Italia

JUVENTUS inatakiwa kuzungumza na Chelsea kama inataka kumsajili Jorginho, kwa mujibu wa wakala wa mchezaji huyo wa timu ya Taifa ya Italia, Joao Santos.

Mabingwa hao wa Serie A, Juve wameripotiwa kutaka kumuunganisha Jorginho na kocha wake wa zamani, Maurizio Sarri hapo Turin baada ya wawili hao kuwa wote kule Chelsea na Napoli.

Jorginho anatajwa kwamba ndiye mrithi anayefaa wa Miralem Pjanic, ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na mabingwa wa LaLiga, Barcelona na vinara wa Ligue 1, Paris Saint-Germain.

Uvumi umeenea na kudai kwamba Jorginho anakwenda Juve na uhamisho wake utamhusisha Federico Bernardeschi ambaye atabadilishana naye.

Hata hivyo, Santos amekanusha kwamba Juve hawajafanya mawasiliano yoyote na Chelsea kuhusu kumtaka Jorginho.

"Mimi nasikia tu huo uvumi na kuandikwa kwenye magazeti, kwa sababu hakuna mtu kutoka Juventus aliyewasiliana na mimi," alisema Santos akiiambia TuttoJuve.com.

"Maurizio Sarri anamkubali sana yeye kama mchezaji, walifanya kazi pamoja, lakini kwa sasa hakuna lolote la zaidi. Yeye ni mchezaji wa Chelsea na kama Juve wakimtaka wanapaswa kuzungumza na klabu yake."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BENZEMA AITANGAZIA VITA BARCELONA LALIGA

## Hatuna cha kusubiri, ujumbe wa Zidane ni tufurahie kucheza soka, tumejifua...

**MADRID,** Hispania

KARIMU Benzema anashawishika kwamba Real Madrid watakuwa wakali zaidi wakati Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, itakaporejea, akibainisha kwamba, kocha wao, Zinedine Zidane amewataka "kufurahia kucheza" baada ya mlipuko wa virusi vya corona.

**Baada ya miezi mitatu ya kusimama kwa msimu kutokana na ugonjwa wa Covid-19, Madrid itarudi uwanjani Juni 14, mwaka huu wakati watakapowavaa Eibar.**

LaLiga imeruhusu kuchezwa bila mashabiki majukwaani na Madrid inajiandaa kuipiku Barcelona kwenye mbio za ubingwa.

Barca wanarudi kwenye msimu huu wakiwa wanaongoza kwa pointi mbili kileleni dhidi ya wapinzani wao hao, lakini Benzema anaamini 'Los Blancos' wapo tayari kutoa changamoto ya kuwania taji la ligi hiyo, huku Zidane akiwahamasisha wachezaji wake kufurahia kazi yao.

Benzema ameiambia televisheni ya Real Madrid: "Ujumbe wa Zidane ni tufurahie. Tufurahie kucheza soka. Tumejifua zaidi kuliko wiki iliyopita.

"Tumejifua kuwa fiti zaidi kwa wiki iliyopita na sasa, na tunakabiria kuanza LaLiga, tumejiandaa vizuri.

"Wachezaji wote wameanza kuzoea haraka kucheza kwa kila hatua. Inafurahisha tukiwa na wachezaji wenzetu, kwa sababu ni ngumu kuanza upya kwa kasi, lakini wote wanaonekana kuwa fiti.

"Miezi miwili bila kugusa mpira, ni jambo gumu kwa mchezaji, lakini sasa tupo vizuri na tunarudi kwa ajili ya kupambana kubeba taji la Ligi Kuu na tupo tayari kwa hilo.

"Hatuna cha kusubiri kuanza mashindano ya michezo yote iliyobaki ni muhimu sana kwetu. Mchezo wetu wa kwanza utakuwa dhidi ya Eibar nyumbani na ni muhimu sana. Hivyo tutacheza kwa bidii kwa dakika zote."

Real Madrid haitatumia uwanja wake wenye uwezo wa kuchukua mashabiki 80,000 katika mechi zilizobaki na badala yake mechi zao watachezea kwenye dimba la Alfredo Di Stefano wenye uwezo wa kuchukua watazamaji 6,000 pale Castilla, kwani Santiago Bernabeu unaendelea kukarabatiwa.

## ZISIKUPITE

### CHELSEA YAMTAKA CHILWELL

CHELSEA imemfanya mlinzi wa Leicester, Ben Chilwell mwenye umri wa miaka 23, kama chaguo lao la kwanza, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa England anaweza kuwagharimu kiasi cha pauni milioni 85. ***(Athletic)***

### ZIDANE AKOMAA NA POGBA

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amezungumza na wakala wa kiungo wa Manchester United, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 27, akisema bado ana nia ya kumsajili mshindi huyo wa Kombe la Dunia. ***(Le 10 Sport)***

### UNITED KUMPOTEZEA SANCHO

MANCHESTER United inamtambua winga wa Velez Sarsfield ya Argentina, Thiago Almada mwenye umri wa miaka 19, kama ndiye mbadala wa uhamisho wa nyota wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20. ***(Manchester Evening News)***

### INTER KUMGEUKIA LACAZETTE

INTER Milan wanapanga kumsajili mshambuliaji wa Arsenal, Mfaransa Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 29, kama straika wa Argentina, Lautaro Martinez mwenye miaka 22, atajiunga na Barcelona. ***(Mundo Deportivo)***

### MILAN KUMSAJILI HENDRICK

KLABU ya AC Milan imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Burnley na Ireland, Jeff Hendrick mwenye umri wa miaka 28, akiwa huru. ***(Sky Sports)***

### HAKIMI JICHO LAKE HISPANIA

WAKALA wa mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Achraf Hakimi mwenye umri wa miaka 21, ambaye yuko kwa mkopo kutoka Real Madrid, anasema kipaumbele kwa mchezaji huyo ni kucheza katika klabu ya Hispania, lakini anadai hakuna haraka kwa mchezaji huyo kutoka Morocco kurejea. ***(Evening Standard)***

### NEWCASTLE YAACHIWA ROSE

KLABU ya Tottenham Hotspur imempa ruhusu beki wa England, Danny Rose, 29, kubakia kwa mkopo Newcastle kwa kipindi cha msimu kilichobaki. ***(Football Insider)***

### BARCA YAIBIPU MAN CITY

BARCELONA wametuma ofa ya kutaka kumsajili tena mlinzi wa kati wa Hispania, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19, kutoka Manchester City. ***(ESPN)***

### GALATASARAY KWA TAYLOR

KLABU ya Galatasaray imeingia kwenye vita ya kumsajili straika wa Charlton, Lyle Taylor mwenye umri wa miaka 30, ambaye hataichezea tena klabu yake kwa sababu mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto. ***(Mail)***

### M'BAYE AWINDWA MARSEILLE

KLABU ya Brighton inaonekana itashindwa kumsajili straika wa Rennes, M'Baye Niang mwenye thamani ya pauni milioni 15, baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, kuwaniwa na Marseille. ***(Star)***

### LONGSTAFF APEWA OFA

KIUNGO wa Newcastle, Matty Longstaff, 20, ambaye kwa sasa anapokea mshahara wa pauni 850 kwa wiki, amepewa ofa ya mshahara wa pauni 30,000 kwa wiki na klabu ya Serie A, Udinese. ***(Sky Sports)***

HABARI MICHEZO

## Klabu Ligi Kuu Z'bar mazoezini kesho

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

JUMLA ya michezo 146 ya Ligi Kuu Zanzibar imebaki kabla ya msimu huu kumalizia ambao umekumbwa na msukosuko mkubwa wa janga la virusi ya corona vilivyosababisha kusimama kwa ligi mbalimbali duniani ikiwamo hii ya visiwani hapa.

Wiki iliyopita Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliruhusu Ligi Kuu tu ndio irejea, huku michezo mingine na ligi nyingine ikiendelea kusubiri hadi itakapotoa tamko.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Mashindano wa ZFF, Ali Mohammed, alisema wanatarajia shughuli za mazoezi kwa timu kuanza rasmi kesho baada ya kukamilika taratibu za afya ambazo walielekezwa na serikali kuu.

Alisema wanaendelea kufanya kazi kwa pamoja na wizara ya michezo katika kujadili mambo mbalimbali ambayo wizara hiyo imetakiwa kutoa mwongozo kwa ZFF ikiwamo taratibu za kiafya hususan kwa wachezaji na viongozi wa klabu katika kuendelea kujikinga na virusi vya corona.

Alisema wanachosubiri kwa sasa ni wataalamu wa afya kutoa elimu kwa viongozi wa klabu, madaktari wa timu, waamuzi, walinzi wa viwanjani na milangoni, waokota mipira (ball boys) pamoja na wafanyakazi wa ZFF husuan wa Kamati ya Mashindano na Bodi ya Ligi ili kuhakikisha lengo la serikali la kujikinga na virusi vya corona michezoni linatimia.

Aidha, alisema suala hilo la kutoa elimu ya afya linasimamiwa na Wizara ya Michezo pamoja na Wizara ya Afya, hivyo ZFF inaendelea kufanya kazi kwa ukaribu na wizara hizo ili kuhakikisha maagizo yote yatakayotolewa wanayatekeleza.

## Kocha Lipuli alia wachezaji kutojifua

**Na Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimebaki siku tisa kabla ya Ligi Kuu kurejea, Kocha Mkuu wa Lipuli FC, Nzeyimana Mailo, amewalalamikia wachezaji wake kwa kitendo cha kutofanya mazoezi wakati wa mapumziko ya lazima yaliyotokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona.

Hata hivyo, Lipuli FC haina kiporo katika ligi hiyo, hivyo itaanza kushuka dimbani Juni 17, mwaka huu katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi kuvaana na Polisi Tanzania, hivyo Mailo bado ana takriban siku 13 za kukiweka sawa kikosi chake.

Lipuli ambayo ipo nafasi ya 13 kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 33 zilizotokana na mechi 29, iliingia kambini Mei 31, na ndipo kocha huyo alipogundua wachezaji kutokutimiza majukumu ya kujifua wenyewe kulingana na programu alizokuwa akiwapa.

"Wachezaji wangu walikuwa hawafanyi mazoezi jambo ambalo linanilazimu kuanza kuwasimamia upya kuweza kuwarejesha kwenye ubora wao.

"Wameanza kufanya vizuri kwa kuwa tumeanza nao mazoezi kwa pamoja, tutafanya vizuri kwani ninajua namna ya kwenda nao sawa kikubwa nimewaambia wanapaswa wajitume," alisema.

# CHAMA KUTUA J'TATU, SHAIBOUB HAIELEWEKI

**Na Saada Akida**

WAKATI kiungo wa Simba, Clatous Chama akitarajiwa kurejea nchini Juni 8, mwaka huu, klabu hiyo imekiri kuwa haifamu ni lini kiungo Msudan Sharaf Eldin Shaiboub atarejea kuungana na wenzake kujiandaa na Ligi Kuu Bara inayotarajiwa kuendelea Juni 13, mwaka huu.

**Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana baada ya mazoezi yaliyofanyia Uwanja wa Mo Simba Arena uliopo Bunju, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sven Vandenbroeck, alisema kurejea kwa Chama kumekuwa rahisi kutokana na Zambia kulegeza masharti ya mipaka ya kuweza kufika nchini kuungana na timu hiyo.**

Alisema kesi ya Shaiboub imekuwa ngumu kwa sababu ya nchi yao ya Sudan kuweka sheria ngumu ya watu kutoka au kuingia nchini humo.

"Chama ataingia Juni 8 na atakaporejea atalazimika kujifua kivyake kwa ajili ya kujiweka fiti kabla ya kuungana na wenzake katika mazoezi ya nguvu, ila kesi ya Shaiboub kuhusu ni lini atarejea, bado ni ngumu sana kwa sababu ya nchi hiyo kufunga mipaka," alisema Sven.

Alisema mazoezi yanaendelea na wachezaji wote wako vizuri, huku akitarajia Francis Kahata na Ibrahim Ajibu leo kuungana na wenzake katika mazoezi ya kucheza mpira.

"Kahata na Ajibu walifanya mazoezi binafsi ya kuwa fiti na wameniridhisha, hivyo kesho (leo), wataanza mazoezi ya pamoja uwanjani na wenzao kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya michezo yetu iliyobakia ya ligi," alisema Sven.

Alisema licha ya kuwa na ratiba ngumu ya mazoezi na muda wa kurejea kwa mechi hizo, wanapambana kuhakikisha wachezaji wake wanarejea katika ubora wake kutetea taji la ubingwa.

Kuhusu Kombe la FA, Sven alisema: "Kwa sasa siwezi kuzungumzia mechi ya FA, kabla ya kukutana na Azam FC kuna mechi takriban nne za ligi, hivyo akili na nguvu zote tunaelekeza katika michezo hiyo kwanza," alisema Sven.

Kwa upande wa nahodha Msaidizi wa Wekundu wa Msimbazi hao, Mohammed Hussein 'Tshabalala' alisema wamerudi zaidi walipoishia baada ya corona.

"Kiufundi kocha ametuongezea vitu, kuhakikisha tunatetea ubingwa wetu kwa kuhakikisha tunashinda mechi zetu zilizobakia," alisema Tshabalala.

Ligi Kuu ilisimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona, na hadi inasimama Simba ambayo itashuka dimbani Juni 14 kuikaribisha Ruvu Shooting katika Uwanja wa Taifa, ndiyo iliyopo kileleni ikiwa na pointi 71 ikifuatiwa na Azam FC yenye alama 54, huku Yanga ikiwa na pointi 51.




Wachezaji wa Yanga, kiungo mshambuliaji Bernard Morrison na beki wa kati Kelvin Yondani (nyuma) wakiwa mazoezini kujiandaa na Ligi Kuu inayotarajiwa kurejea Juni 13, mwaka huu kwa timu hiyo kuvaana na Mwadui FC katika Uwanja wa Kambarage mkoani Shinyanga. **PICHA: YANGA**

## *Singida yaapa kutoshuka daraja*

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara inayotarajiwa kurejea Juni 13, mwaka huu, Klabu ya Singida United imesema kuwa imejipanga kisawasawa kwa mechi zilizobaki na ina uhakika kuwa haitoshuka daraja kama wadau wa soka wanavyodhani.

Mkurugenzi wa klabu hiyo, Festo Sanga, amesema baada ya ligi kuruhusiwa kurejea kufuatia kusimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, wameanza maandalizi kabambe kuhakikisha wanafanya vema ili kujinusuru kwenye janga la kushuka daraja.

Alisema kitendo cha Ligi Kuu Tanzania Bara kuchezwa nyumbani na ugenini kimewapa matumaini ya kufanya vema mechi zao hasa za nyumbani ambazo watahakikisha wanaondoka na ushindi ili kuifanya timu hiyo isishuke daraja.

"Bado tuna mechi nyingi ambazo tukicheza karata zetu vizuri, basi tunasalia Ligi Kuu na kuna watu wengi wanadhani kuwa tutashuka daraja, lakini nawahakikishia mashabiki wa soka, pamoja na wakazi wa Singida, kuwa tumejipanga kisawasawa na tunafanya maandalizi ya kutosha kwa ajili ya urejeo wa ligi. Hata ukiangalia kwenye mechi yetu ya mwisho kabla ya ligi kusimamishwa, tulishinda kwa mabao 2-1 dhidi ya Mbeya City, kwa hiyo tutaanzia pale tulipoishia," alisema Sanga.

Singida ina mlima mrefu wa kujinusuru kutoshuka daraja, kutokana kuburuza mkia, ikiwa na pointi 15 baada ya kushuka dimbani mara 29, ikisaliwa na michezo tisa ili kumaliza msimu.

# Michezo

Alhamisi Juni 4, 2020

Nipashe




Benzema aitangazia vita Barca

UKURASA 22

HESABU...



Kiungo mshambualiaji wa Simba, Luis Miquissone (kushoto), akipiga hesabu za 'kumzunguka' beki wa timu hiyo, Shomari Kapombe, wakati wakiwa mazoezini jana katika uwanja wao wa Mo Simba Arena uliopo Bunju jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba SC kutangazia ubingwa Nangwanda

## ●●● Sven ageukia utimamu wa mwili, asema siku 10 zilizobaki zinatosha nyota wake kuanza...

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, akieleza kuwa ameisoma ratiba ya Ligi Kuu, lakini wachezaji wake hawajawa tayari kwa upande wa utimamu wa mwili, hesabu zinaonyesha mabingwa watetezi hao wanaweza kutangazia ubingwa wao wakiwa ugenini watakapocheza dhidi ya Ndanda FC kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara Julai 5, mwaka huu.

**Kwa sasa zimebaki siku 10 kabla ya Simba kucheza mechi yake ya kwanza tangu Ligi Kuu Bara ilipositishwa Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa homa kali ya mapafu, Covid-19.**

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa Jumatatu wiki hii na Bodi ya Ligi (TPLB), Simba itacheza mechi yake ya kwanza katika Uwanja wa Taifa dhidi ya Ruvu Shooting Juni 14 ikiwa ni siku moja baada ya watani zao, Yanga kuvaana na Mwadui FC katika dimba la Kambarage mkoani Shinyanga.

Na baada ya mechi hiyo, Simba ambayo ina pointi 71, huku ikihitaji alama 14 tu ili kutangazwa mabingwa kwa mara ya tatu mfululizo, Juni 20 itaialika Mwadui FC katika Uwanja wa Taifa kabla ya siku nne baadaye kuivaa Mbeya City katika dimba la Kumbukumbu ya Sokoine na kisha Julai Mosi kuivaa Tanzania Prisons kwenye uwanja huo.

Kama itavuna pointi hizo 12 katika michezo hiyo minne, Julai 5, mwaka huu itaifuata Ndanda FC ikiwa na lengo moja tu la kutangazia ubingwa Mtwara, wakati itakapohitaji ushindi ili kuruhusu mashabiki wake kuanza kusherehekea ubingwa huo wakiwa Mtwara, huku wakibakiza mechi tano dhidi ya Namungo FC, Mbao FC, Alliance FC, Coastal Union kabla ya kuhitimisha na Polisi Tanzania katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi hapo Julai 26, mwaka huu.

Pointi hizo 14, zinatosha kuifanya Simba kufikisha alama 85 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote Ligi Kuu Bara msimu huu, kutokana na Azam inayoshika nafasi ya pili kwa sasa kuwa na pointi 54 huku timu hizo kila moja ikibakiza mechi 10, hivyo ikishinda mechi zake zote itafikisha alama 84.

Hata hivyo, pamoja na kukiri wachezaji wake kutokuwa tayari, Sven amesema wiki mbili zinatosha kuwarejeshea wachezaji wake utimamu wa mwili tayari kuanza mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Sven alisema kwa sasa bado wachezaji wake hawako tayari kurejea kucheza ligi kwa sababu hawana utimamu wa mwili kutokana na kukaa nje ya uwanja kwa muda mrefu, lakini siku zilizobaki kabla ya kushuka dimbani, zinamtosha kuwarejesha kuwa fiti.

Alisema kinachohitajika kwa sasa ni muda zaidi wa kufanya mazoezi ya pamoja ili kurejesha utayari wa mwili, stamina na kasi kabla ya kuanza mikikimikiki ya ligi siku 10 kutoka sasa.

"Nitaendelea kubadili mifumo ya mazoezi kwa kadiri muda unavyozidi kwenda ili kuwaweka tayari wachezaji kabla ya ligi kurejea kwani tuna wiki moja tangu tulipoanza kujifua.

"Ratiba nimeiona, ukiniambia kuwa kwa sasa tupo tayari kucheza nitakwambia hapana, kwa sababu wachezaji hawana utimamu wa mwili. Kwa hizi siku zilizobaki kabla ya ligi kurejea zitatusaidia kutuweka vizuri na jambo zuri ni kwamba asilimia kubwa wachezaji wote wako kikosini isipokuwa wawili tu," alisema Sven.

## Kocha Yanga avurugwa akiwa Ubelgiji

**Na Adam Fungamwango**

SAKATA la Kocha wa Mbelgiji wa Yanga, Luc Eymael kushindwa kurejea nchini, limeendelea kuchukua sura mpya, baada ya kubainika kuwa kuna watu 'wasiojulikana' walimvuruga kwa kutumia ujumbe kuwa klabu yake ina mpango wa kumtema ndiyo maana hawajamtumia tiketi ya ndege, huku makocha wenzake wa kigeni wote wakiwa wameshawasili nchini Tanzania kuendelea na kazi zao.

Hayo yamebainishwa jana na Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alipoongea na Nipashe, juu ya maneno aliyoyatoa kocha huyo akiwa nchini kwao kuwa anakerwa na tabia ya viongozi wa klabu hiyo ya kumcheleweshea tiketi na haelewi nini kinaendelea.

Bumbuli alisema kuwa kocha wao aliongea maneno hayo kwa presha, kwani kuna watu walimpelekea taarifa kuwa kuna mpango wa kumsitishia mkataba wake, wakimweleza kama Yanga wangetaka arejee wangeweza kufanya hivyo mapema kwa sababu makocha wenzake wote wa kigeni tayari wamesharejea nchini kuendelea na kazi.

"Tumemtuliza na yeye ametuletea meseji za watu ambao walikuwa wakimpelekea na ndizo zilizosababisha aongee maneno hayo. Kila kocha anatoka kwenye nchi yake na kila moja ilikuwa na taratibu zake za kukabiliana na corona, na si wote wanatoka Ubelgiji, lakini ukweli ni kwamba yote yamekwisha na mambo yakienda vizuri tarehe sita atakuwa ameshawasili nchini," alisema Bumbuli.

Akijibu shutuma hizo, Ofisa Habari huyo alisema kuwa awali kabisa kocha wao alikuwa na tiketi ya kwenda kwao Ubelgiji na kurudi, lakini kutokana na dunia nzima kukumbwa na ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona, safari zilifutwa.

"Mwezi Aprili pia tulilipa dola 8,000 kwa ajili ya tiketi, lakini anga bado zilikuwa hazijafunguliwa na ilipofika Juni Mosi, tulianza mchakato wa kumtumia tena tiketi, lakini ikumbukwe ndiyo wakati ambapo safari nyingi za ndege zilikuwa zinaanza na anga kufunguliwa kulikuwa na safari nyingi, hivyo siku tatu nzima za mwanzo ndege zilikuwa zimejaa, ilibidi tufanikiwe kukamilisha tiketi za kuanzia tarehe nne," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >